Ya mwisho ni ya kwamba wa kristo, waangalie Bibilia sana wasije wakiingiza siasa, wanawake pia wale wameolewe mimi nasema saa hii, nikiwa hapa mzee yule mwanamke ameolewa aheshimu bwana wake. Tunataka kwa ofisi ya serikali tu akifanya kazi jioni akirudi ajuwe bwana yuko. Kwa sababu hii imeleta matatizo kwa watoto wetu kwa sababu mama anafikiria anataka kuchukua kila kitu, kila kitu halafu sasa katika Bibilia inasema mwanamke ako chini ya mzee, na mzee ako chini ya serikali sasa kwa nini mama anataka kuwa juu ya mzee halafu tugawanye mali sasa tunaelekeza watoto wetu wapi kwa sheria? Lazima tuelekeze watoto kwa sheria ya kusema mama aheshimu mzee na kazi yake achunge mzee wake. Ya mwisho wazee, wazee waangaliwe nchi ingine wazee wakiwa miaka 75 wanapewa nafasi kukaa katika wengine wanaumia kama yule amesema hapa

saa hii, ameumia lakini sasa apewe, wazee kama hana mtu wakumchungwa bona walemavu wanachungwa na wazee kwanini akiwa hana mali yoyote kwa nini serikali haiwezi kuchungwa tunataka wazee wachungwe. Asante sana.

Com.Nunow: tafadhali, hatuwezi kuendelea namna hii, hii sio heshima na siwezi kuendelea namna hii, ukiambiwa umalize time zako zimekwisha, tunataka uheshimu na usimamie hapo, kama utaweka microphone kwa mdomo kwa sababu unapiga kelele atasikia, haitakusaidia na haitasaidia mtu yeyote, na hatuwezi kuendelea namna hiyo nawambia. Kama mnataka tuweke nidhamu ingine ya kushika mtu mkono na kuondolea, tutafanya hivyo, lakini hiyo ni mbaya, tuwe na heshima ukiambiwa time yako imekwisha time yako, imekwisha. James Muruu.

James Muruu: Asante sana ninafurahia sana, jina langu ni James Muruu Ekital, hasa nimekaaa Trans-nzoia karibu miaka 23. sasa siwezi sema mengi kwa sababu inakubukwa tu pahali akilala vile ninakaa hivi ninakubuka pahali ya kulala jioni, kwa sababu hakuna shamba hakuna pahali a kulala, mtu anakaa sijui tu kwa barabara tu. Ninakaa kwa barabara hapa tu, sina pahali pa kulala, nikitoka tunaend kibarua asubuhi kwa watu kupalilia lakini vile ninakuja hapa ninakumbuka pahali pa kulala jioni. Mtu ni maskini tu pahali watu wanaita squatters halafu ndio wa kwanza ma squatter hawo, maanake sina pahali pa kukaa. Ndio mimi sasa sina mengi yangu yaishia hapo.

Com.Nunow: Tafadhali James andikisha pale jiadikishe pale, Ebonyo Enyaman, baada ya Ebonyo, Lochamin Ebenyo pia ajitayarishe.

Ebenyo Enyaman: Asante ndugu wangu, mtume wa sheria na wananchi. Asante (inaudible) jina langu Ebenyo Enyaman. Kila kitu abacho kimenileta hapa unajua sana, sana, wale watu ambao wanaumia zaidi kwa hapa Kenya, E-Turkana, ndio wanaumia zaidi. Maana yake sina shamba, sina mahali pa kukaa ile kitu ambayo kinaumiza sisi ni hiyo. Kwa sababu hata akikaa kwa shamba ya mtu mtoto wangu akifa, hakuna pahali ya kuzikwa, bibi yangu kama akifa, hakuna pahali pa kupeleka kwa Municipal. Hivyo ndio unaumiza wa Turkana zaidi, mtume wa sheria. Kama madadiliko ya sheria, inakuja sababu ya hiyo sheria ndio ninasema wa Turkana wanaumia zaidi kwa serikali hii. Unaona hapa wa Sabaot wanatetea upande wa Wasabaot wajua nini wanaona shida yao, ndani ya maisha yao, lakini sana, sana, mtume wa sheria, pande ya wa Turkana zaidi kuwapa Kenya hii. Sina mengi ya kusoma, nishukrani kwa Mungu, Mungu akubariki.

Com.Nunow: Asanti: Lochomin, ajitayarishe James Kaptipin.

Lochamin Ebenyo: Kwa jina ni hiyo Lochomin Ebenyo. Kwa hivyo hakuna zaidi ya kusema, kile kitu nitasema ni hivi, nataka sheria ile itatuendesha mbele katika Kenya. Sheria ile iliyotuendesha iliyotuendesha kutoka Kenya, kutoka wakati wa Kenyatta ile sheria alikuwa anasema tufuate, iko wapi hiyo, sheria hiyo iko wapi? Kwa kusema kweli tunachagua kweli wako? Hakuna kitu wanafanya, akija anafanya kwake tu peke yake, lakini kwa sisi, ni watu ambao tunaumia wale unaweza sema wako Kenya, kura kupigwa inakanyagwa kweli. Lakini hakuna kazi ile anafanya, sisi wale watu tunafanya mimi hakuna mtu ninachagua,

akasema hii, na hii, sisi tu wenyewe, wenyewe sisi wenye kuharibu sisi wenye kujenga, kwa maana hakuna ile tutasema, ningetaka leo kukuambia wewe, utuangalie sisi vile sisi wa Turkana tuko hapa. Kwa hivyo watoto wataweza kusoma kwa upande wa ukulima kwa jembe, watoto kama wako kama tano au sita na wote wanasoma, tutafanya namna gani, tutawasaidia namna gani, vile sisi tuko namna hii., chabulia kura ikija tuko pamoja, sisi wenyewe, sisi tunaharibu nchi yetu kwa masomi kwa kufanya nini, sisi wenyewe, hakuna mtu anatoka Tanzania, sisi wenyewe. Wenyewe sisi wenyewe tukae pamoja sawa, kwa hivyo yangu ni hayo. Mungu awabariki.

Com.Nunow: Asantr sana tafadhali jiadikishe. James, Kapipin

James Kapipini: Asanti Commissioner, kwa nafasi hii kwa jina naitwa James Kapari basi kuna mambo matatu nitagusia, kuhusu Katiba hii. Mimi ninatoka katika jamii ya Sengwer Cherengani. Kuhusu ardhi, sehemu hii ya Trans-nzoia wakati wa koloni walipofika, walikuta jamii wawili, hawa ni Sabaot na Sengwer Cherengani. Na hawa walikuwa wanajua mipaka zao ,basi Bwana Commissioner, hawa jamii wanajua wa koloni wa gapi walinyakuwa sehemu ya ardhi ya wa Sabaot na wa jamii na wazungu wagapi walinyakua sehemu ya jamii ya Sengwer Cherengani. Na vile tulivyopata uhuru, hawa jamii wawili hawajafaidika, katika sehemu zao ambao wakoloni waliwanyang'anya. Basi tungetaka Katiba iweze kuangalia hawa kwa sababu iliwasahau. Lingine ni kuhusu mambo ya ubunge, katika sehemu hii, ambayo ilikuwa ya jamii ya Sabaot ama Cherengani ipate kuangaliwa, kwa sababu utakuta hawa hawajafaidika hata kidogo, tangu uhuru mpaka wakati wa leo. Kwa mfano utakuta Constituency ingine ya Cherangani Constitutuency, lakini hiyo Constitutuency haiwasaidii hawa jamii wa Sengwer Cherengani. Basi ningependelea Bwana Commissioner Katiba iweze kuangalia hawa, jamii yote ipate uakilishi katika bunge ya Kenya.

Basi la mwisho ni kuhusu muda wa Tume. Ninaomba Bwana Commissioner, mpewe muda wa kutosha kwa sababu hii ni maisha ya jamii wa Kenya. Kwa sababu ukikatiziwa muda, isipotengenezwa Katiba ya kusaidia jamii yote, basi Katiba hii hatutafaidika. Asante sana.

Com.Wanjiku: Keba Balua yuko,

Keba Balua: Commissioners jina langu ni Keba Balua, nataka kuzungumzia au kupendekeza juu ya mipaka ya nchi ya Kenya. Mipaka hii ya nchi ya Kenya, imechangia wananchi kutoka katika nchi jirani kuingia nchini humu na kunyakuwa udongo wa nchi wanaingia na silaha na kufanya wananchi kuwa na uoga. Nataka pia kusema, police, GSU, wanakasoro, zinafunza hawa officers kutokuwa na imani na wananchi wa kawaida. Wanatoka huko wakiwa na tabia za majivuno na kuweza kutishia wananchi mala, kwa mala wanapokuwa katika utekelezaji wa kazi zao.

Nataka kusema juu ya mashamba, mashamba nchini Kenya itoke katika ofisi zifuatazo, katika ofisi ya Rais mashamba yatoke huko, katika ofisi ya PC, mashamba yatoke huko, pia kusiwe na Commission of land. Badala yake mashamba yote yale katika

ofisi ya PC, na Location ya chief itekeleze wajibu huo.

Jambo lingine ninataka kusema juu ya sheria ilioko ya urithi wa mali kutoka kwa wazazi. Kushtaki kaburi ndipo uweze kuchukua shamba hili la mzazi linamatatizo makubwa, kwa hivyo mambo ya kushtaki kaburi la baba ndipo uwe mrithi yaondolowe na mambo haya yachiwe familia na location ya chief.

Jambo lingine nataka kusema ni kwamba, katika Katiba yetu ya sasa, itengeneze idara ya kubambana na ufisidi nchini. Ufisadi umezidi na kila mmoja angiambo ofisi anaananza kupanga jinsi atanyakuwa mali ya nchi au mali ya wananchi kwa ujanga mbali, mbali, kwa hivyo ufisadi umezidi sana. Nataka pia kupendekeza ya kuwa Katiba ya sasa ikumbuke wazee wa mitaa na itengeneze budget kwa ajili ya hawa wazee.

La mwisho, maskini na watu walio viwete na viziwi, na watu wa namna ile nyingi, serikali iweze kuwaangalia na iweze hata kuweza kuwapatia marupurupu ya kila wakati maana nao imekuwa mzigo kwa wale ambao wanawatunza.

Com.Wanjiku: Thank you very much, Wesir Mukoya,

Wetir Mukhoya: Mimi mwenyewe naitwa Wehir Mukhoya mkaazi wa Trans-nzoia. Na maoni yangu vile ninapendekeza maoni, tulikuja kwa maoni sisi hatukuja kwa siasa, siasa iko baadaye. Miaka yangu naona ndio nilileta uhuru, wacha nipendekeze yale ninayo machache na mafupi. Mapendekezo yangu ya kwanza machief wachaguliwe kwa mlolongo, raia waende kwa mlolongo. Kuongezea hiyo ya wapili, wanawake wanaolewa na watu, ng'ombe kumi na tatu na mbuzi tatu. Mila ya watu ni mwaafrika yoyote kupendekeza, kuongezea yale unaona mwanamke anakushtaki kortini ati munawachana na hawo watoto tulizaa na hawa, hiyo kuwe mkazo.

Ingingine wanasema ya kwamba kuficha mambo ya wazee, siku hizi Kenya iko huru, wazee wacha nitoboe sisi wazee kitu ambao wanasema sisi wazee wakongwe kama sisi namna hii namna hii tunataka pombe ya mrija, ya mrija ya kurengekha. Sio Chang'aa mtu asifiche Nairobi, Kenya mzima tunaona mrija iko hiyo ikubaliwe. Na mwaka huu, tunaona mwaka huu tunatahirisha watoto. Kutahirisha watoto kuna watu ambao watatahirisha wana kisu kwetu. Tuliona siku hiyo wakitahirisha mtoto hakukuwa na ugonjwa, mwenye anatahirisha mtoto anachukua licence kwa serikali ati lete sheria ya kutahirisha mtoto, hiyo ikomeshwe.

Jambo lingine naona watu wengine wanateua, mnaishi hapa Kitale, Kitale kuna sehemu yake, na mimi mwenyewe vile ninaona, mtu anakamatwa anawekwa ndani ya rumande, wakati ya kortini kuja kuona mtu wako na chakula askari wanapewa pesa ndio mtu akubaliwe kuona mtu wake. Kweli tabia hiyo Kenya watu wako huru kweli? Hiyo ikataliwe, tunaona na macho, kama hutakuwa na pesa hutaona mtu wako kwa chakula.

Ingingine naongezea mtu akichaguliwa akienda kwa bunge akienda kwa bunge wanananchi wa Kenya, akienda kwa Bunge,

katikati ya kama anaongoza vizuri aendelee kwa hiyo miaka, kama hapana endelea vizuri raia wapige kura waweke mwingine huyo akae nyumbani. Kitu ingine mambo ya Rais wa Kenya, Rais wa Kenya achague wazee ambao corner yote wale wanamshauri, ajue wazee wako kwa corner Kenya. Sitaki kuwachoza nataka kuwa mahali ingine, ingine, nasikia kengere nina heshimu wazee kama nyinyi. Yangu ni hayo tu.

Com.Nunow: Mark Kisenbe, ajitayarishe Sylvester Wanyama,

Mark Kisenbe: Commissioners ladies and gentlemen I have a paper here majina ni Mark Kisenbe. The paper consists of fundamental points to consider when reviewing the the Constituion of Kenya. The Commissioner the Constitution needs to have a preamble to cater for the aims and objectives of the Constitution. Under the directive principles of state policy, this paper Mr. Commissioner, recommends that the new Constitution should contain a preamble and a directive principles of state policy stating how power should be exercised for instance the head of state, Legislature, Executive and Judiciary wing. In the system here must be having the state control. I will only highlight on the points that I have on the paper and present it as a memorandum.

I also talked about the Constitutional Supremacy. I have concentrated my efforts on the citizenship of this country, because I feel, the citizenship of this country it's a fundamental factor of a state. Every person who having been born in Kenya, shall become a citizen of Kenya. That which pertains the statutory instrumental 1963, and the gazetted paper of 105, of the order that chapter one should be adopted. I only exempt the dual and women citizenship here. It is properly detailed in that section Mr. Commissioner.

The defence and National security, the paper has examined a number of details here. Under defence and national security Mr. Commissioner, the armed forces, air force, navy, should be established by the President as an institution enshrined in the Constitution. Internal security should have an appropriate Ministry which will deal with internal affairs.

Under political parties Mr. Commissioner, we are suggesting or I am suggesting this that we have in all democratic fairness all parties belong to one camp with single objective, that is the struggle for power. Look at the situation in Kenya today, now any party in Kenya does not have an ideology, so we are suggesting this one, that any party will run its own affairs.

Under the structures and systems of the government, we have suggested a number of the government that will assisted but empasize on the establishment of unitary system of government.

Under Executive, we have examined a number of factors to be considered, especially the office of the President the office of Prime Minister, and the office of the MP in the Parliament and the life of the Parliament.

Under Judiciary Mr. Commissioner, we have looked at the number of the courts, on top we need to have the Supreme Constitutional court and below it will have the Juvenile dealing with the status of children in the country.

Finally now Mr. Commissioner we have proposed that we include or we create a new Province, that is North Rift Province, consisting of the following Districts, ie. Keiyo, Marakwet, Turkana, Trans-nzoia, Nandi consisting of a new Province in this paper. I have left the owner Mr. Commissioner, to present this as a memorandum to the Commission. Thank you very much.

Com.Nunow: Thank you very much Mr. Kisembe for those views and the memorandum Sylevester Wanyama, after Sylevester Councilor Muliro jitayarishe.

Sylevester Wanyama: Dear Commissioners, my names are Sylvester Wanyama and I am speaking on behalf of Trans-nzoia self sponsored University students and we have outlined in our paper, we have looked at two issues one of which is the structure and systems of government.

Interjection Com. Nunow: Mr. Wanyama just a minute. Please settle down first because you are obstructing and destructing at the same time. If you have settled we can continue.

Wanyama: We have noted that in heteretenious society like Kenya, unitary system of government just do not work. We have noted that highly Centralized Unitary government constrict liberty, reduce freedom all round, and create speeds environment for sleazy operations, and embezzbement corruption, graft, sound, arrogancy, incompetent leaders in government and many other evils. It is in the right of this observations that a federal system is proposed for Kenya in this treatise. As a way out of tyranny and instead to extend democracy to all. We have therefore proposed that the levels of our federated republic of Kenya should be under a very basic level called the village council and then rise up the county authority which will be a coup of associated village councils, it is the local government of an area occupied by a sub-tribe. An autonomous state this is a group of associated county authorities thus the government of the entire tribe and there after we shall at the apex, the federated publics of Kenya. The federal republic appears to be a stable a state where, powers of the government are so effectively decentralized to other bases, thus to the Constituency states. Our beloved Kenya has some very large tribes like Abaluhya, Kikuyu, Luo Miji-kenda, kalenjin Maasai kamba etc. Each of which occupies a large and defined territory, federation we are sure, would provide for and contain their different peculiarities, then best power sharing with the village councils, county authorities, and the state should give the two political stability in Kenya, which will be difficult to disturb. The entire Provincial Administration system, from the Provincial Commissioner down to the assistant chief, should be replaced with elected representatives of the people, through regular, free and fair elections held at intervals of every two years.

We concurr with the structurer arrangements and organizations of the village councils county authorities, urban councils and Municipalities and Constituency states as outlined by P.H. Okondo in his book, "a commentary on the Constitution of Kenya of

Our argument for the creation of tribes states are, tribes states provides checks and balances which are very difficult to disturb as I have pointed out. Tribes are the foundation of nationalism, it must be understood that to belong to a tribe, is not a negotion of Nationalism but the confirmation of the same. Federation means equal opportunity for all tribes, our proposal should not be equated with tribalism or taken as calculated designs to improve the lot, of any one tribe over the others. On the contrary we propose here to improve the lot of all the tribes nations contemporaneously. Mr. Commissioner sir, we have come a long way for 39 years and we have tried to build up a unitary system of government and this has resulted into tribal clashes, the continued projection into national life of the undesirable tribal balancing at the national level. That is why we hear issues of Kamatusa, we hear issues of Gema, we hear issues Saboit etc. The un ending struggle by each tribe to capture the Presidency for its own economic benefit. The resultants continous rows in the population, government arrogancy and growing degradation of the economy.

Lastly Mr. Commissioner sir, we have also talked about land and property rights, just a minute please, and we have said that land should belong to respective states. Therefore the highest registry of the land should be at the autonomous state level, and therefore there should be no land available for Presidential allocations. Lastly Mr. Commissioner sir, the landowners right to sell or to develop must be un hampered, the Government or local authorities may acquire for austensible specific public purposes only, provided it is fully compensated for to the owner. Kenyans should own land within their specific states.

We again strongly propose that the Constitution should provide for a cealing and land owned by an individual say at most 50 acres, and we have also proposed the creation of the seat of the Prime Minister, a deputy Prime Minister then we have proposed the President and two Vice Presidents. Thank you Commissioners.

Com. Nunow: Thank you Councilor Muliro, Josephine Simiyu.

Josephine Simiyu: Commissioners, Ladies and Gentlemen my names are Josephine Kadogo Simiyu and I have come here to present my personal views, as Kenyan acitizen and a worker in this country.

My views will be on the public service. The new Constitution should state clearly that the public servants are servants of the people, but not Masters of the people as it is in the old Constitution. Let a DC be a servant of the people, but not a Master of the people where people where pay homages and sent delegations to get favours. The Public Service Commission should be appointed by the head of the government but should have the approval of Parliament, to avoid anomalies. The Constitution should guarantee civil servants the right to form association and unions to protect and promote their interest. The union must be protected, so that they do not experience the interference and manipulation that has characterized the central organization of the trade unions COTU. The leadership of such unions should be open to all people i.e. to say men and women and disabled

persons. The public servant should work anywhere in the republic as it has been, but I propose that some form of consultation and dialogues, take place before transfers of the same. The rights to retire on time, and with immediate benefits should be guaranteed in the Constitution.

Retrenchment must be done in orderly just and way and after getting the Parliament approval. People should not be retrenched and they end up dying before getting any benefit because of the urgency with which they are issued the letters.

When the Public servant retires at the age of 55, years they should not be allowed to return to government employment in a new capacity, eg. paramount chiefs, when you retire you go away and enjoy your benefits, then let the new qualified blood take over. This one will reduce the unemployment of our young people. Let them also enjoy their retirements and also allow and stay at home as consultants, but not to draw money again from the treasury. Thank you.

Com. Nunow: Thank you very much Josephine, please register yourself Mary Imuria, is Mary there, Barasa, Makhanu,

Barasa Makhanu: *Asante Commissioner, Khushughuli nicho khushugulika chino khuombakhe sibala, nitaongea Kibukusu tu, babukusu, nga nekhumenya mu-Trans-Nzoia muno,*

Interjection Com.Nunow: Excuse me just a moment, gentleman excuse me, excuse me, you what is the problem? We deal with our responsibility yours is to come and bring views, please do not have heart for yourselves, okay, we do not want anybody's excitement hear, we said in the morning anybody is free to speak any language and the translation is the Commission's responsibilities, is that clear? Lets just relax continue please.

Barasa: *Asante Commissioner Khukhwicha khukhwimelela khu mukanda kwo khwicha na khuandikisia, ne kamasina kase bananga bali Baraza Makhanu Namwinguli.*

Translator: Thank you very much Commissioners for you coming here, to listen to us. My names are Barasa Namwinguli.

Barasa: *Salwa musibala sia Sayuni mu Trans-Nzoia muno.*

Translator: I was born in the land of Zayuni in Trans-nzoia.

Barasa: *Nga nesalwa vikuka ne vikuka byaolela muno.*

Translator: As I was born our ancestors and their ancestors, were right from here.

Barasa: *Nibyo khuuka, kumwaka kwa elfu moja na mia nane samanini na tatu, basungu ne bakhaira mu Trans-Nzoia*

...

Translator: What surprises me in the year 1883, when the Europeans were killing us, in Trans-nzoia here,

Barasa: *Kumwaka kwa elfu moja na mia nane tisaini na tano, ne becha khaira ... muchingo chiefwe cha Trans-Nzoia chino bakhairira mu sikulu sia Chetambe.*

Translator: In 1895, when the Europeans came here to take over our residents in the port of Chetambe they were killed their.

Barasa: *Kwaba ne chingoba munalamanjalal, nende sirikwa nende mulwendebe.*

Translator: We had ports here in Majelala, in Sirikwa and in Endebbes.

Barasa: *Nende Ndalwa nende mungo mwa kitalia muno.*

Translator: Ndale and in this home of Kitalia.

Barasa: *Basungu bano bama khwicha, kumwaka kwa elfu moja na mia tisa mbili, ne becha khukhutibaicha ne bakhuonakaka.*

Translator: In 1902 when the Europeans came here to divide us and spoil us.

Barasa: *Bama khukhuonakaka khubela khwaba nende omwami wefwe mumia, khukhwama sibala sie emwalo eino ne khucha mpaka Naivasha.*

Translator: They spoiled us because we had our leader Mumias, from this land upto Naivasha.

Barasa: *Ne Mumia niye waba oruka sibala sino, ne khukhwama emwalo ebuko nende emwalo.*

Translator: Mumia was the leader of this land from the East and the West.

Barasa: *Kumwaka kwa ishirini na sita, ne bakhurakho, khukhurakho flu, ne khukhulasimisha basungu ne banywa chikhafu chie kamabele kefwe.*

Translator: In 1926, we were forced to cut some certificates called blue and the Europeans forced us to give our animals and extract the milk from our animals.

Interjection Com. Nunow: Could we hear what his recommendations are, pendekezo.

Barasa: *Mbendekeza ndi kumpaka kwe kamajimbo kataru, khwenya Sano, nend Kirinyaga nende Mfano khukhwama Mombasa nende Nairobi nende Sano Musayuni.*

Translator: That he is recommending federation, three federations i.e. the Coast region, the Central region and the Western region.

Barasa: *Ne khulondekhana ne bukekke bwe buibwami, nio balanga bali omwandiki omukhulu wa angaki, nende olondelakho khubwami omukhongo, abe Mombasa, no wa akarikari abe Sano, ne President abe akarikari we Kirinyaga, namwe mujimbo liosi liosi linyolekhane.*

Translator: so he is proposing the leaders, the senior most leaders should be central and then another leader in the Coast another one from the Western region.

Barasa: *Ne bubwami bwene obwo, sekhwenya bubwami bwe khu..ba –advocate mubarusie khu mikunda.*

Translator: that those leaders should not have the power to distribute land.

Barasa: *Mulekehe basakhulu be engo nende babami be engo.*

Translator: it should be left to the local leaders in the villages, and the regions.

Barasa: *Ne liokhuuka sana, nga bajirane balomile bali sibala khucha wae ne waena, so khumali sikila bebatisie barie ta.*

Translator: although surprising some people were trying to say that other communities must leave it does not understand, where those communities should go.

Barasa: *Ne sikulu sino sia masaba nisio.*

Translator: that this mountain is Mount Masaba.

Barasa: *Ne masaba ino, yabadalisha eriri nende omusungu bali Argo, kumwaka kwa hamsini, -elfu moja mia nane nahamsini, Argo na saveya sibala sino.*

Translator: that there was an European called Argoi in 1850, who changed the named from Masaba to another name I do not know.

Barasa: *Nga nekachenja Victoria nende Brodrick falls, nende kai...*

Translator: Just like the Europeans were changed Lake Victoria the Fredrick falls and what have you.

Barasa: *nande Mt. Elgon, nende Thompson falls*

Translator: that this Mt.Elgon and Thompston falls were the creation of Europeans.

Barasa: *Khubela omusungu wa khukalukhasia. Asante.*

Translator: Thank you.

Com.Nunow: Thank you Christopher Mughasia. Christopher Mughasia five minutes p please

Christopher Mughasia: Asante sana Commissioner kupata nafasi hii, jina langu ni Christopher Mutasia kutoka Kinyoro. Na hili ndio pendekezo ambalo ilitolewa na ma squatter katika location hiyo. Ya kwanza, mashamba makubwa yapunguzwe ili mtu anaye miliki acre za chini, iwe ekari kumi. Na mashamba ya matajari makubwa, makubwa, yapunguzwe na wasio na makao waweze kupata.

Ya pili majina ya watu, wenye wamepewa mashamba iwe computerized, ili isaidie kuwatabua wale wanaopata mashamba hapa, na pale. Kuna matajiri wengine ambao wanapata mashamba ukienda Uasin Gishu yeye yuko, ukija Trans-nzoia, yeye yuko, kwa hivyo ikiwa itakuwa computerized na mtu awe na shamba tu sehemu moja katika nchi hii, itawezesha wengi kupata mashamba.

Sheria ya urithi wa ardhi, ya marehemu iondolewe kortini na irudishwe kwa kamati ya vijiji ya kiendeshwa na ukoo. Kwa sababu mambo ya advocate na kwa wale wa mama wajane huwa ni shida sana, kusafiri Nairobi ama wapi. Kwa hivyo ikiwa kwa vijiji, itawezesha wao kuweza kupata nafasi. Uwezo wa ugawaji wa ardhi uondolewe kwa ofisi ya raisi, na mashamba yarudi kwa kamati maalum ambayo itachaguliwa na wananchi katika sehemu hiyo hiyo, hiyo shamba iko.

Kamati isiwe inachaguliwa kutoka District nyingine kuenda kupeana ugawaji wa mashamba katika District nyingine, hapana, iwe tu ni katika sehemu hiyo katika location hiyo, mahali hapo, hapo, hiyo ardhi imepatikana.

La mwisho, ma squatters tuwe na uakilishi, tuwe na mwakilishi mmoja katika nchi nzima ya Kenya kwa kuwakilisha masirahi ya ma squatter katika idara ya serikali. Tunaona ya kwamba wale watu wasio na makao wameweza kujukuliwa tu kama machokora katika street. Wanapopeana maombi yao ya kupata mashamba, hayo yanakuwa covered na matijiri wenye mifuko minono, na hii inazidisha umaskini katika nchi yetu hii, na ndio sababu mnaona kila mala tuko na tatizo ya mashamba, lakini mashamba yako, utaratibu ukifuatwa kila mtu atakaa vizuri hatutaomba, omba misaada kutoka ng'ambo. Asanteni kunisikiza.

Com Nunow: Asante sana, Simon Musamia, after Simon ajitayarisha Enock nyukuli.

Simon Musamia: Asante sana Bwana Commissioner mbele yenu ni W. W. Musamali nikiakilisha jama ja Fanu African National Union, yani, Zayuni African National Union. Hiki ni chama ambacho kilikuwa cha babu zetu tangu awali, walipoingia wakitoka misri mwaka 1470. Waliingia katika mlima Zayuni, na walipofika katika mlima zayuni, Bwana Commissioner tungelipenda kupendekeza leo kwamba nchi hiyo yetu ya zayuni irudishwe na mipaka zake zote, kwa sababu ilimilikiwa kutoka Jinja hadi Naivasha. Na wale watawala, na wale watawala ambao walitawala alikuwa ni (inaudible) akiwa wa kwanza hadi wa 32, akiwa Mumias wa Nabongo na aliondelewa ofisi tarehe 12 mwezi 11, ikiwa 1926 wambebelul wakibadilisha nchi yetu, na walipo badilisha nchi yetu bwana Commissioner ilikuwa na tarehe moja mwezi wa nne mwaka 1902, hiyo ilikiwa na siku ya ujanja, kwa hivyo mfahamu kabisa nchi ilinyakuliwa lajambavu.

Bwana Commissioner ningelipenda kuendelea nikikwambia kwamba mashamba yetu, ambayo yako ndani ya Trans-nzoia ni mashamba ambayo tungelitaka ya milikiwe na jamii yenyewe ya wa Bukusu. Hii tamaa, bwana Commissioner ningelipenda kukwambia ukweli kwamba kutokea mwaka 1932, wakati alipoulizwa kutoa maoni yake na Commissioner aliye chair hiyo Commissioner alikuwa Minister (inaudible) na alipoulizwa kutoa maoni yake, son of Masaba alionyesha kabisa ya kwamba, mfalme Mumia aliwatawala kutoka Jinja hadi Naivasha na alikuwa na vikosi maalum ambapo mtu asije kutudanganya sisi ikiwa hajasoma historia vizuri, arudi katika chuo kikuu na achukuwe mamlaka ya kusoma vizuri.

Bwana Commissioner ningelipenda kuendelea kwa haraka tu kuhusia juu ya squatters. Mambo ya kuwa squatters sisi tulikuwa settlers wa Trans-nzoia tokea hapo awali, na tulipokuwa settlers mtu ambaye alileta ndio tuitwe squatters alikuwa na mkoloni ama mbeberu. Na wakati alipoingia, alipambana nasi huko Lubeka, shebabe na Marale Sengeri mpaka Naivasha huko kwa (inaudible). Wakati huo wote, tulipigana hizo vita na tulipopigana tuliwashinda vita, tukaua wazungu 42, walikuwa 58 tu ndio walinusurika na waloporudi kule kwa king George, aliwatuma warudi tena tupigane nao na tulipambana vilivyro, kama askari wetu na interior walifany kazi ya kuweza kufanya mambo ikakuwa mbaya huko mahali panaitwa Ruboka na Chitambe, ndio mbukusu akaimba wimbo (kiluhya dialect.....) ningependa Bwana Commissioner, uchukuwe kabisa na

ufahamu kwamba hapa tuko na mlima wetu wa Zayuni, ambao kila mmoja atauona vizuri ha huyu ni mlima ambao tuko hapa, hapa karibu na ambapo sisi sasa wabukusu tukirudi kwa desturi zetu, wametufungia kupeleka maombi yetu katika mlima huo, na pendekezo ni kwamba, waondoe kabisa wajibu wa kutufungia kupeleka maombi katika mlima huo, ili tufanye maombi ambayo yalikuwa yakifanywa na babu zetu ili hali zetu za msambura ziendele kumiliki na kuhakikisha upepari ulitoka katika nchi yetu.

Bwana Commissioner, ningelipenda pia kupendekeza mamlaka ambayo Rais Moi ako nayo yashushwe ili juu ya haya yote yeye asisimamie mashamba kwa sababu juu ya mashamba imetuadhili sisi hasa wa Trans-nzoia kwa sababu vivo vya viongozi wetu kama Maside Muliro, George Katil hata Mayor Shitachi wamekufa na wale watu ambao wamekuwa wakiwaua, wamepewa ardhi kama zawadi pade hii, acre 1,500 na zaidi. Ningelipenda kupendekeza tena hivi, Bwana Commissioner, kwamba sisi kama wabukusu tuko na desturi yetu ambao huwa tunafanya wakati watoto wanaona, wakati watoto wanatahiri, ni hili inaruhusu tuwe tunatumia tembo yetu ya busaa, kwa hivyo wote wakubaliane nasi kwamba busaa itakuwa ni pombe ya desturi.

Bwana Commissioner nikimaliza, ningelipenda serikali ambayo tunachukua sasa, ili kuwe katika Katiba hii mpya, iepuke damu. Ikifanya kazi yake, ifanye ikijua ya kwamba bila binadamu ama bila mwananchi hakuna serikali. Bwana Commissioner ukichukua number ZA yani Nzoia peke yake ukichukua neno Nzoia uchukue halafu ubadirishe, uchukuwe Z, A, I, O, utapata inasoma Zayoni kwa hivyo nchi hii ni yetu na hatutaki hata nchi ya jimbo letu, moja ipotelee nje. Asante sana Bwana Commissioner.

Com.Nunow: Enock Nyakuli, Enock Nyakuli ajitayarishe Nyongesa Iadi.

Enock Nyakuli: Asante sana Commissioner, mimi ni Enock Nyakuli wazee hukumbuka.

Interjection Com. Nunow: Can we have silence, please if you have any business to discuss, you will do this process a lot of justice by going out, finish and then come back.

Enock Nyakuli: Mimi Enock Nyakuli, kutoka Kimilili wazee hukumbuka. Mambo yangu ni mengi, lakini mara ya kwanza, tumetoa mapendekezo yetu, na mambo yetu ambayo tumeyaandika tumepeana. Kwa hivyo mimi sitakuwa na mambo mengi zaidi isipokuwa ndani ya karatasi yetu, tunataka utawala wa ma-chief urudi kwa raia wawe ndio wanachagua, si kwa ajili ya kupitia kwa interview. Hiyo mambo inasumbua sana. Neno lingine kama mbunge tumemchagua kwenda bunge na kama hahudhulii na kuleta report nyumbani mikutano, atolewe tuchaguwe mtu mwingine maana hana faida na sisi.

Neno lingine, kama Councilor, tumemchagua councilor, ameenda kazi na yeye hahudhuria mikutano na kuleta report nyumbani tunataka arudi kama raia hata tuchague mtu mwingine aende aakarishie nchi yetu. Maana kuna shida sana upande wa viongozi

wetu, tunawachagua hakuna kitu ambao wanaweza kutufanyia.

Mambo ingine kama upande wa rasimali ya area hapo au mashamba, mashama ya area hapo, inatakikana irudi kwa county council, na county council iwe na wazee wa hapo, hapo ndio wajue wale ambao wako na shida maana squatter inapatikana kwa ajili watu wengine wanatoka mbali wanachukua mashamba, na wenyenji wanakosa mashamba, ndio tuko na shida ya ma squatters. Neno kwa ajili ya Trans-nzoia vile wengine wameongea, kuna mambo iko, tunataka wale ambao wanasema nchi ni yetu, tupatiwe nafasi halafu tutoe kila mtu atoe sababu yake, halafu tujue nchi ni ya nini. Maana wengine kwa sababu wengine wanasema tulifukuzwa tukaenda Uganda, tukaenda wapi, ndio tumerudi mlikuwa huko wapi, sasa ni miaka idadi wakati tulipata uhuru ni miaka mingi wewe ulikuwa wapi mpaka wakati wa sasa? Ndio wanasema nchi hii ni nchi yangu, nchi yako kwa njia gani? Kwa njia gani, tunataka tujue, tukae na tuulizane, tutoe sababu ya kutosha ikiwa ni nchi yenu tujue, kama ni nchi yetu tujue, lakini unajua hii nchi yetu hii Trans-nzoia na nchi ya wa Bukusu, asante.

Com.Nunow: Nyongesa endelea.

Nyongesa Iadi: Asante sana mimi naitwa Nyongesa Iadi, nikiwa mkaazi wa hapa Trans-nzoia, ni mwenyeji wa Trans-nzoia, na vile wengine wamesema kama ni Mungu, Mungu anajua niko hapa na sababu gani. Mimi ningependa kupendekeza kwamba Provincial Administration iwe scrapped na badala yake, tuwe na strong Local Government, ambayo itakuwa na Elected representatives, Mayor ama County Council Chairman, awe mtu yule anachaguliwa directly na watu wa area hiyo. Na awe mtu ambaye ana kiwango kizuri cha elimu. Siyo degree, lakini awe mtu ambaye anaweza kuthibitisha kwamba anaweza kusimamia mashirika, yaani ako na Administrative capacity ama managerial capability ya hali ya juu. Atatoa CV yake kwa nominating authority, na hiyo CV lazima watu wa area wajue yeye ana uwezo gani wa kufanya kazi.

Kazi ya police katika mpangilio huo itakuwa chini ya hiyo authority. Mayors, ili tupate ma Mayor ama chairman wale walio na elimu nzuri watapewa mshahara mzuri ili kazi hiyo iheshimiwe. Mshahara uwe kama ule wa ma MPs wabunge. Chiefs na ma sub-chief wawe wachaguliwe na wananchi. Ma chief officers wa Local authority wachaguliwe na Local Authority, lakini public service Commission ithibitisha. Mayor lazima awe na official residence. Kama hapa Kitale, kuwe na nyumba ambayo itakuwa ya mkuu wa area hii na aishi hapo. Hapana mtu kutoka area fulani anaishi huko, lazima apewe authority na residence, na ofisi ya Mayor itapeana hiyo uzito, wa mtu kuwa amechaguliwa mahali pale na akatoka kwakwe aende aishi kwa hiyo residence.

Minister wachaguliwe kutoka kwa ma Professionals, wasiwe wajumbe katika bunge. President asiwe Member wa Parliament, achaguliwe direct na wananchi na awe na running mate wake. Parliamentary na Presidential elections ziwe tofauti na zile za local government. Local government election ziwe tofauti ili, wananchi waweze kuchuguzwa wanachagua nani katika Local Authority.

Jambo lingine ningependa kupendekeza ni kwamba harambee, official harambee ziwe abolished. Development ya hii country ya

hii nchi lazima itoke kwa ushuru, from taxation. Kwa sababu mambo ya ma harambee ndio imeleta ufisadi mkubwa. Pesa zile zinachangwa kwa harambee hatujui zinatoka wapi, ni za wizi. Leaders wote, ukitaka kuchaguliwa kiti chochote, lazima useme mali yako umetoa wapi, ili tuchague watu wale wako na nidhamu hapana wezi waje kuwa viongozi wetu, asanteni sana.

Com.Nunow: Asanti Rev. Nelson Cheleget. Atakeyefuatwa na Stephen Tedet.

Rev.Nelson Cheleget: Mimi ni Rev. Nelson Cheleget, nina mambo machache sana, kwanza point la kwanza mila na desturi ya kila kabila iwekwe ndani ya Katiba vizuri. Na jambo lapili wa Sabaot na Sengwer warudishiwe mashamba yao, walionyanywa na serikali ya ukoloni zamani.

Jambo la tatu, Trans-nzoia kwa jina la Cosmopolitan, ziondolowe kabisa, jina hilo huleta ufisadi na unyakuzi wa ardhi. Hiyo iondolowe kabisa, iwe tu Kitale.

Point la nne, Land Control Board, ifanyiwe na wazee wa nyumbani. Wazee ndio wanaofahamu vizuri sana ya kwamba nani asiye na shamba, ni nani ni mwenyeji wa hapa. Kuliko mtu kutoka nchi ya mbali na anakuwa mwenyeji wa kugawa yale mashamba.

Jambo la tano, Katiba ihakikishe kila kabila ndogo inawakilishwa bungeni. Imekwisha wakilishwa bungeni. Katiba iwekwe kila kabila ndogo makabila haya 42,iwe ya kwamba imekwa imewakilishwa bungeni.

Jambo la sita serikali ya majimbo ianzishwe ili maendeleo ya karibu yafikie wananchi. Na Na point ingine la saba tangu multi-party system, tuliona mambo mapya sana wakati wa multi-party system jinsi watu wa Kenya wanavyotaka kuishi. Tumeona kila kabila ndogo ama kubwa walitaka kutambuliwa kwa nchi yao. Kwa hivyo mipaka itambuliwe vizuri kufuatana na kitabu cha Mungu inasema katika Deutronomy 33 kuanzia 7 na 8 hiyo mipaka iwekwe vizuri kabisa. Na uongozi pia na kila kabila na pia Bungoma na Wangoma kwa sababu wale ni nchi ile watambuliwe vizuri kikatiba iwekwe ndani ya Katiba, Bungoma, kwa sababu Bungoma ni wangoma hiyo iwekwe vizuri kila mmoja anajua, sio mambo ya kusingizia, iwekwe vizuri katika Katiba ya kwamba nchi ni ya wa Sabaot.

Na jambo la nane Mt.Elgon District ingizwe katika Rift Valley ije katika hii Rift Valley ingizwe mlima wa Elgon ije Rift Valley Mt.Elgon District. Na jambo la mwisho chief wa kwanza wa hapa Kitale Bana Kitale Arap Kesis, iwe tunadai serikali kuweka account ya rubies 3,000, na hivyo anastahili ajengwe ijengwe hospitali kwa niaba ya jina lake. Na pia shule ua ufundi kwa jina la heshima la chief Arap Kesis, na ni hayo tu ambayo ninasema. Thank you Commission.

Com.Nunow: Asanti sana Rev. tafadhali jiandikishe pale kwamba umetoa maoni, Stephen Tedet.

Stephen Tedet: Asante sana Bwana Commissioner, maoni yangu ni kitu kidogo sana lakini mimi naomba wewe usikie kwa makini. Majina ni Stephe Tedet. Ya kwanza ndio hii ukweli unahimiza watu wengine kwa nini mtu asikubali ukweli wa kitu. Kitu mimi ninasema anahimiza ukweli ndio huu kwa kusema Trans-nzoia ni ya nani kila mtu anasema ni yangu. Na ile kitu utaleta Trans-nzoia kuwa kama Rwanda, hiyo ni haki, na tena mkirundi nyumbani ama mkirudi Nairobi ama huko, mjue nyuma iko tabia kwa nini ndio hii chunguza ama rudi tena halafu itakuwa wazee kutoka kila kabila. Halafu tuendelee pole, pole tujue Trans-nzoia, ukweli uko upande wa nani.

Kitu ingine sisi hapa Trans-nzoia tunaumia watu wa National Park wako hapa, forests iko hapa na hakuna kazi ya kutusaidia sisi katika Trans-nzoia, ama sisi wenye tuko karibu na National Parks. Na watalii wanakuja kila mara ama kila miaka, miaka hii yote na hiyo pesa zuna kwenda kujenga mashule ya nje. Na sisi tunaumia hatuna barabara, hatuna mashule, hatuna ma hospitali hatuna vitu vingine vyo vyote. Watoto wetu wanakalia mawe na sisi tunalinda miti mbao, mbao inakwenda Webuye na sisi hapa hatuna Factory yeyote ingelikuwa zile mbao zingetusaia.

Kuna kitu ingine hapa Trans-nzoia, jina la Trans-nzoia lilikuja na mzungu, na mzungu alisahau jina yake ya kurudisha, sisi tunataka hilo jina la Trans-nzoia liondolewe bali. Sasa hakuna haja ya kusema kueleza nini hii ni nafasi yangu. Trans-nzoia ilikuwa watu karibu mbili, Sengwer, Saboit upande ule ni watu wa Pokot, ndio walikuwa wanatawala, na Gajoni upande ule tena. Uhuru wa Kenya tangu mwaka wa 63, Sabaot hawajui uhuru ni nini na wengine wanasema at Sabaot walikwenda wapi, walikwenda wapi walingweda lini Uganda, nani alikuwa anaishi na mzungu, na mzungu alikuwa mkali yuko na bunduki yake na nani ndio alikuwa anaishi na mzungu, na mzungu. Through learning wakati mzungu alikuja chai ya kwanza ama maziwa ya kwanza yalikuwa ya Msabaot. Kwa ndume ya ukulima ulikuwa ya wa Sabaot zilikuwa iko wapi hizo kabila zingine. Ng'ombe zote zilikuwa hapa zilikuwa za Sabaot na hao waliokoa ng'ombe kuenda Uganda, na wengine wanakwenda Narok, wengine wanakwenda Tanzania na akirudi anasema ni mgeni, mgeni wa wapi, tutaongea na tutapata ukweli, na ukweli utabaki na ukweli wake.

Com.Nunow: Asanti sana tafadhali jiadikishe, Godwin Oganya, of St. Joseph Boys Kitale.

Godwin Oganya: My name is Godwin Oganya from St.Joseph's Boys Kitale representing the students from that school. I am going to read it in English.

On Education the government should provide free education for all children upto the age of 16 years, to reduce the number of street children. It should be compulsory for parents or guardians, to take their children to school. The government should also ensure all street children are taken to school.

A (inaudible) should be put in place to cater for the educational needs of children. The Local authority should build and locate schools in their respective areas. They should provide modern laboratory equipment. This is to prevent movement of students

upto far areas in such of schools with better facilities. Those incharge of the Local authority in a given area should have at least a post secondary education. The government should provide milk to cater for nutritional needs of children.

Technical subjects should neither be scrapped in Primary nor in secondary, this has helped a great deal in the jua kali sector of scrapping out means people will not be creative enough.

On the side of discipline legal notice number 56 of March 2001, outlaws canning of students in schools replacing it with guarding and counseling. This has had advance effect increasing unrest in schools. The government should deploy professional guiding and counselling personnels to schools and also look for a way of involving parents in their children's discipline.

Stern actions should be taken against on children involved in drug abuse. The government should allow free tests to anyone suspected to have taken drugs under the supervision as a counsellor. Education Minister should be in full control of education. He should be responsible for safety of students in schools. He should ensure competent people run the schools.

On environmental conservations every citizen has a right to live in a clean environment. Any one found throwing litter anyhowly should be punished. Owners whose vehicles emit a lot of smoke and noise should be penalized for polluting the environment. Factories should not litter harmful gases to the atmosphere or chemicals to water bodies, to conserve the marine life and for a clean environment. For every tree cut down, we should ensure that at least two should be planted for a healthy environment and it should be put in the Constitution. Thank you very much.

Com.Nunow: Excuse me Godwin, please you can go back to the mic, give us your age and form the class.

Godwin. I am Godwin Onganya from St. Joseph's Boys High school Kitale I am 18 years of age and in form four.

Com.Nunow: Florence Nangila, Joseph, Ngaruiya

Joseph Ngaruiya: Asante sana Bwana Commissioner na wananchi kwa siku hii ya maoni. Mimi jina langu ni Joseph Ngaruiya natoa maoni kwa niaba yangu. Kwa habari za barabara, na uchukuzi ningelipendekeza, serikali ya Kenya iondolee mbali habari ya kupeana contractors lakini itumie Ministry ya public works kutengeneza barabara zetu na kurekebisha kwa sababu itagharimu fedha kidogo na uchumi wa nchi hautaidhinisha sana. Hivyo, hivyo ningelitaka pia Engineers wale watakuwa wakipitisha barabara, ambazo hazijajengwa vizuri, waweze kuwekwa ndani kuanzia chini ya mwaka mmoja na wasiweze kufanya tena katika nchi hii yetu. Na pia kama magali yataweza kupata accident kwa sababu ya mashimo, itakuwa ni kwa sababu serikali imeshindwa kutekeleza wajibu wake, itaweza kugharimia wale ambao wameumia na kutengeneza magari hayo.

Upande wa afya ya wananchi, ningelitaka ya kwamba wana nchi waweze kupewa huduma ya matibabu bure pasipo cost

sharing. Na kusiwe na habari ya kwamba kuna madawa ambayo ni ya bei ghali, wananchi waweze kugharimia la sivyo, serikali ichukue jukumu lote la madawa na matibabu. Na kama kuna matibabu ambayo inaitwa special treatment, inatakikana kupelekwa katika nchi za nje, hivyo serikali iweze kugharimia matibabu hayo kwa wananchi wa Kenya. Na kama madaktari watachalia mgonjwa kwa kumpa labda madawa yaliyoisha mda ama kutowatibu kwa njia inayofaa, daktari huyo awekwe ndani, na asifanye tena kazi katika nchi hii yetu, kwa sababu afya ya wananchi wetu lazima iangaliwe vizuri.

Katika ofisi za serikali public offices tungeitaka ya kwamba masaa yao ya kazi yaweze kuangaliwa vizuri sana. Kama ni saa mbili, saa mbili kamili wawe wemeingia katika ofisini na wa hudumie wananchi. Kuna wakati mwingine kunahitajika form kujazwa katika ofisi za Serikali, badala yake hao ma officer wanafanya kazi ya serikali, kuamba wananchi waweze kujijazia, hatutaki namna hiyo waweze kuuliza wananchi maswali na wenyewe waweze kuwajazia kwa sababu wanalipwa kazi hiyo.

Upande wa elimu tungeitaka elimu iwe bure, iwe ya bure free primary education. Na katika upande wa secondary school, tungelitaka ya kwamba wale ambao hawana fedha za kuweza kutosha kulipa, waweze kupea bursary na iwapo mtoto wa tajiri anaweza kulipiwa bursary kinyume cha sheria, yule tajiri aweze kulipia wanafunzi maskini wa nne na iwe ni sheria hivyo.

Na upande wa kilimo tungelitaka ya kwamba serikali iweze kuondolea ushuru, kwa bidhaa zote za kilimo na kama kunaweza tokea habari ya janga kama vile ukame, serikali iweze kuwapa wakulima mbegu, fertilizer na wawape pesa za kuweza kulima pasipo kutozwa chochote. Ni hayo tu Bwana Commissioner

Com.Nunow: Asante sana tafadhali jiadikishe Morris Wangus, karibu.

Morris Wangus: Commissioners ambao mmekuja siku ya leo nimeshangaa sana leo ni siku ya Njonjo Commission ama na Constitutional Review, kwa sababu wenzangu wanakuja hapa wanaongea juu ya mashamba na mipaka lakini leo nikuongea juu Kenya inatakiwa iwe namna gani. Fine majina yangu ni Morris Wangus Makhoha, nakaa hapa Kitale na nitaongea tu kwa mambo machache, I shall be very brief.

Kitu cha kwanza Mungu ama vile sisi tulizaliwa Kenya hii, ama duniani hakuna mtu alituma barua kwa mwenyezi Mungu ya kusema mpaka nizaliwe mkalenjin Mluhya, mkikuyu ama nini, tulijipata Kenya and we should co exist as one people in this country. Let me just come to my point straight, wacha nije kwa mambo ya Constitution na mambo sheria.

Vested in the Presidency, appointment of the Parastatal chiefs, are you getting me right Mr. Commissioners, appointments of Parastatal Chiefs, should not be vested in the Presidency and I have a reason to say why. Ama nitarudisha (inaudible) viongozi wa mashirika ya serikali, viongozi ma MD, wasiwe wakichaguliwa na Rais, nikikana na haya, ni hivi. Tuko na Public Service Commission kazi yake ni nini? Makamu huyu kwa sababu Rais ataangalia rafiki yake aseme Moiben ni rafiki yangu sana yeye asimamie several brooke board. Moiben hatafanya kazi ya raia, atafanya kazi in the interest of somebody who appointed him,

of which as a result cereals and produce board itaangukaa na wakulima wanaumia.

Number mbili, hayo lazima tuko na parastatal nyingi KFA, wale wanasimamia wanachaguliwa na Raisi. Hatutaki kitu, hawa watu wanasimamia wachaguliwe na Raisi, wachuguliwe na panel under the supervision of Public Service Commission. Hata niko na wasi, wasi kwa sababu wale watu mnasimamia Commission Chairman Yash Pal Ghai alichaguliwa na Rais, I do not know whether you are doing the right thing. We are afraid tunaongea tu, lakini hatujui.

Number tatu Bwana Commissioner hizo powers itolewe kwa Rais kabisa irudi kwa Public Service Commission, Public Service Commission uchukuwe watu fulani ndio wana check hawa watu, ni nani anafaa kuwa kwa KFA, ni nani anafaa kuwa Kenya Seed, na nini anafaa kuwa kwa Cereal Board, na nani anafaa kuwa wapi, na wapi, ili Kenya iendelee vizuri.

Number nne, suspension of Parliament or any Council in Kenya if it is under the powers of the President to do it? Bado mimi nasema hivi

Interjection Com.Nunow: Please give us your recommendations.

Morris: Basi mimi nasema namna hii, kwa sababu Rais pia ni mjumbe, hana ruhusa ya ku suspend Parliament, anenda any council suspend anaenda wapi ana spend tunataka tuwe na special nini ikiwa council yoyote inafanya makosa ama nini tuwe na special forces ndio inakaa chini ku-suspend na uki-suspend especially hapa Kitale tuko na problem sana. Ma councilors hawa walikuwa suspended under which law. Was it after which Commission, was it a directive ama ilikuwa nini. Sasa kwa hayo machache, nataka tuangalie kwa hayo mambo, tuchukue mambo fulani, fulani ati tuweke kwa mtu mmoja na kusumbua mambo.

Com.Nunow: Namuita Wekesa. Wekesa, Ekenga. Imeandikwa vibaya kwa hivyo Wekesa K. Box number 1971, what is your box number? What is your box number sir? Now that is not you. Stephen Makali kwa sababu kila mtu anaambiwa ajijazie form wengine wanaandika jinsi ambavyo haitasomeka, Stephen Makali.

Stephen Makali: My names are Stephen Makari so I just wish to give my personal views, how I want to admit that most of the views have been given by other people. But I want to re-emphasize the fact that in our next Constitution, there should be democratic principles. I want to propose that never should there be the example that was proposing in Mlorongo. All voting election should be done by secret ballot. I also want to propose that there should be unity, and stability principles and that never should we be having situations where people come to claim, individual or tribal issues, those ones do not instill unity and stability. We want to live in a united environment, whereby everybody should have a right or merit, to own what he may own.

On economic principles, I want to propose there should be an institution to curb economic blunder, something like for example

the office the Audit and Controller General should be independent. Tenure of office must be independent, such that these people must do their work properly and with independence, and appointment must be on merit.

I also want to propose, gender issues in our new Constitution, that languages for example which discriminates against people who are vulnerable like women and what have you, should be taken care of in our new Constitution.

Human rights: I want to propose that certain human rights should curb discriminative tendencies because we normally see that when people claim, for example people claim that this is our region and whatever, at the end of the day, there are things like tribal clashes, and these once here sometimes have caused people to suffer a great deal. So in our new Constitution, there should be entrenched institutions which curb such kind of tribal discrimination.

On foreign policy we want to emphasize on the fact that, we should only be having people dealing with Kenyans. Our foreign policy such as sometimes our boundaries some people have sneaked in, some people from across Uganda have sneaked in and at the moment he comes in here, they claim citizenship and begin causing trouble.

On government and systems, Mr. Commissioner sir I wish to propose that in this country we should cease calling people squatters, you know somebody who has squate, like if we are sitting in this room the way we have sat like, if there was somebody who was squatting here, he cannot sit as long as now, so calling people or “Chokoras” or destitutes in this country 39 years after independent, that one is very discriminative and very dehumanizing. Such a people squatters, or chokoras and what have you in this country, there are enough resources, and they should be taken care of through whatever means social welfare and what have you.

Also finally, I wish to propose that anybody working anywhere or doing anything should not be given a right to appraise his own payment. For example the way the members of Parliament were trying to appraise their own salary, that one in our new Constitution should be curbed so that we should use a body which will give such kind of appraisal. I wish to say more Commissioner, but because of time, I wish to thank you again.

Com.Nunow: Thank you very much please register yourself, Councilor Muliro.

Councilor Muliro: Commissioners my name is Mwashu Muliro Councilor Mwashu Muliro, Cherangani. I wish to say I do not have much, I will not bore you, and I wish to say that what we want and what we must have in our country Kenya, by all means is Peace, is Love, is Unity we have to live together as we are old people and all tribes. Unless we do that, it will be a reputation of the same all things day in, day out on or year in, and year out. Let us have that Peace, let us have that love, let us still have that unity. Also it does not mean that democracy is to undermine what the majority has to undermine the minority.

We have to also safeguard the (inaudible) through majority against the minority. I think those views are enough, I think as for

me that is enough to digest, because we have to think through that. Thank you very much.

Com.Nunow: Councilor, you will be brought the register no its okay, let the register go there. Peter Wanyonyi.

Peter Wanyonyi: Jina langu mwenyewe naitwa Peter Wanyonyi Yakaa, kutoka katika Kitengee area, Kitale:

Maoni yangu, ningependelea ofisi ya Rais ipunguziwe uwezo maana hiyo ofisi ina kazi nyingi sana. Zimekusanyika ndani yake kabisa. Wizara nyingi zimekusanyika ndani yake hata imekuwa na uzito, hata inataka kuvujika, na kuanguka chini. Hizo wizara zingine, zapatiwe mawaziri na ziwe katika nchi zikitumiwa na mawaziri kwa uwezo wao.

Halafu number mbile, upande wa elimu shule za upili ada ama fees, ipunguzwe. Maana hii fees huwa ingine inakuwa nzito sana hata kwa wazazi. Inapandishwa mchana na usiku, ambao wazazi wengine maskini hawewezi kujimudu na ni ma elfu ya pesa. Hata katika vyo vikuu, hizi pesa ni nyingi sana, kwa wazazi wale maskini.

Upande wa vitabu, za shule za msingi text books, hivi vinanunuliwa kila mwaka,wazazi wananunua vitabu hivi kila mwaka, na hivi vitabu, zinatakikana vipewe mda wa miaka mitano, ndivyo viwe expired halafu ndio wazazi wanunue vitabu vingine. Maana hasa hii wizara ya Markit Singh hii sasa imekuwa kama ni biashara tu hata havina maana.

Tatu, ningependelea wizara ya Katiba, idhinishwe iwe wizara maalum katika serikalini. Maana hii ni wizara ambayo inatakikana iwe katika serikali, sio Parastatal, ama namna hivi ilivyo, na ichapishe vitabu vya Katiba ambavyo wananchi wa kawaida wanaweza kusoma na kuelewa Katiba ya nchi yao.

Mkuu wa Sheria achaguliwe na raia, asichaguliwe na President na awe mtu ambaye amesomea hiyo sheria ya kazi yake. Mkuu wa elimu, Makamu wa Rais, pia chaguliwe na raia.

Maskini wengi hawana mashamba, uhai mashamba mengine yana lala bure. Bunge kutuka mishahara minono na hali nchi haina fedha za kutosha inakuwa bankrupt, katika bunge ikaihirishwa kwa mda jee, namna gani na hii bunge ijao itafanya kazi yake namna gani? Maana hii bunge ijayo ya nane itaadhiriwa kwa maana imeingia, haitafanya kazi yake vizuri, maana huu muda wake umekwisha.

Watu walioiba pesa za nchi hii na kuweka nchi ya nje, hizo pesa zirudishwe ili ziimarisha uchumi wa nchi hii.

Com. Wanjiku Kabira: Asante sana David Wamalwa, David Wamalwa, hayuko Wekesa Rosakia.

Wekesa Rosakia: my names are Wekesa Rosakia I am resident of Kiminini Location, and I am here on behalf of those

residents. The hounarable Mr. Chairman and Commissioners of the CKRC, ladies and genlemen. The honourable Mr. Chairman, Commissioners and Ladies and gentlmen, we the residents of Kiminini Location, Kiminini Division of Trans-nzoia District are most privileged to present our views before your most distinguished commission today. We will present it with very special emphasies, on the chief's authority act. Sir following the prolonged struggle for democracy by the Kenyan people, which came ahead in 1997, the inter parties, Parliamentary groups IPPG introduced certain changes to the Constitution and ordinary laws of the republic of Kenya, meant to impact on the rights of all Kenyans, Kiminini residents inclusive. Unfortunately all changes by and large have never been implemented by the Provincial Administration either because the chief had intentionally failed to do so, or the public is not aware of the content of such changes and it does not insist on their implementation. Sir it is as a result of this, very sharp prevailing situation that we the down trodden residents of Kiminini location wish to submit our views as here under:

Proposala amendements about the chiefs. That the chief's authority act be scrapped altogether reviewed and be remained simply as the chief's act. The term authority be removed. The chief should be elected directly by residents of their respective areas of the jurisdiction. Being eligible for re-election after every five years. That incase the government maintains the current trend, then chiefs must be transferred to serve all over the republic like all other civil servants, after at most three years in a particular location. That chiefs who do not deliver qualified services to the residents must not be transferred to other stations, but should still should simply be removed from office. That corrupt chiefs or all those who recruit private armies masquerading as vigilantes in effect harassing residents, and breaking the law with impunity, must be punished accordingly. Those uniforms should not make them appear more equal than any other Kenyan. Mr. Chairman, we have enumerated about 16 amendments to the Constitution regarding the chiefs, but since I will represent this I wish to go to another amendement which we propose to save time.

My personnal views Mr. Chairman, is about the President. I suggest that the national President, head of state, be elected by an overall majority. In the even of the combined vote, of the losers exceeding that of the winner, then a re-run be conducted between the first. The minimum age, for the Presidential candidate be specified in the reviewed Constitution and the age limit, i.e the maximum age of a serving President also be identified. To live office even if he is still popular to avoid having a senile President in office.

The President to serve a maximum of two terms, the President to serve a maximum of two terms of five years each, but must be re-elected through the ballot and not by sycophanoy public opinion. He must not be an elected MP for a particular Constituency. Thank you very much.

Com.Wanjiku Kabira: Thank you very much Mr. Wekesa please sign your name in our register. Benjimin Kitiyo

Benjamini Kitiyo: Asanti sana Commissioners nafikiri ya kwanza aina ya serikali ile sisi tunataka katika Jamuhuri ya Kenya,

kwa sababu hiyo lazima tuweke kwa Constitution ile pia sisi, kwa jina ni Benjamin Kitiyo. Serikali ile sisi tunataka ni ile ya federal Government maana kwa lugha ya kiswahili ni majimbo. Kwa sababu hiyo itakuwa karibu na watu. Kila mahali kutakuwa na jimbo, na watu wengi watafanya karibu nyumbani, na hawatashughulika kwenda kule Nairobi.

Ya pili ni maneno ya land. Land question hata nyinyi Commissioners wenyewe mme witness mnaona watu badala ya kuzungumza hii na ile mpaka kwa land question. Sisi tunaishi hapa Trans-nzoia na tulikuwa tukiishi zamani sisi ni watu Wasabot wamesema mengi juu yake. Nafikiri nyinyi Commissioners mtakuwa na kazi nyingi kwenda kukaa chini na mwaangalie, sababu kama hii Commission itafanya kazi yake bila kuchunguza vizuri, inaweza kuharibu ile sheria au Katiba, Katiba inaweza kuharibika, sababu kila mahali watu wanalia land ilichukuliwa wakati wa wa koloni, na sasa wenyewe wamerudi hatuwezi kusema kwamba kama vile wengine wanasema ati kabila ingine waende, hiyo ni lugha ovyo. Kenya itakuwa namna gani? Watu wakawe lakini sisi tunata utawala, tunataka kuwa na MPs, tunataka kuwa na councilors, tunataka kuwa na chiefs, lakini watu wanakaa kwa mashamba kama vile wako, kwa sababu tukisema watu waondoke hiyo ni lugha sisi hatuelewi, sababu hata sisi tumekaa kwa nchi za watu wengine. Tulikuwa tumekaa huko vizuri, ingawa nchi ya mtu ni mtu na tena itakuwa kwa nchi za bali kama Uganda, Tanzania sasa tumerudi, tunajua watu lazima pamoja, lakini mahali watu wanamenyana, mahali clashes zinatokea, ni utawala peke yake, si yale maneno walisema ni Multi-party hiyo siyo, ni utawala. Kila jamii inataka wawe na watawala wao, ndio hata uliona kijana moja alisema, watu wa Commission wangeenda kwa watu, kwa groups sio mahali watu wanakutana kabila mingi, wengine wanasema hiyo, wengine wanasema hiyo, wengine wanasema hiyo, hata sasa hata anapoteza hata Commissioner's kichwa sisi wa Saboit tunataka kutawala hapa Transo-nzoia na tuweke jina.

Trans-nzoia yenyewe sisi wenyewe tunaita Koing, unaona hiyo jina ya Elgon, hiyo jina El, hiyo ni Kimaasai na huko mbele ni Scory, sasa ilikuwa ni mlima wa Scory, ndio ulisema El Koing, sasa kwa shauri ya miaka mingi ya kubadilika, badilika, watu wakasema Elgon, hiyo GON hata hakuna maana, pengine mkiongeza pengine W, El Koing pengine itakuwa mzuri, sababu ni mlima wa Scory, Koing ndio wenyeji. Sasa watu wengine hawajui kwamba hiyo Elgon ilikuwa ni Mzungu aliyekuja 1883, ndio aliuliza wa maasai upande wa Uasin Gishu. Ile ni milima ya nani, ndio wa maasai wakasema ile ni El Koing maana ile ni mlima wa Koing, ndio hata andika namna hiyo. Halafu ili watu wa Kenya wawe pamoja, kwa sababu tunataka, tunataka tukae pamoja na tufanye kazi pamoja, tugawanye vitu sawa, sawa. Tugawanye vitu vyetu viwe sawa kila kabila iwe na kila kitu, wajumbe, sawa, watu hawa wa kutawala hawa, utaona hata hii maneno ya kufutana na kufuta, hakuna kufutana hii imeletwa na hii kitu kidogo, kidogo kama hiyo.

Halafu serikali kwa sababu ni ya majimbo, lazima wachunguze mishahara ya watu, mnaona hata police wanachukua pesa ya watu njiani, wengine wanagoma, hatutaki maneno ya kugoma, lazima serikali ijue ni kitu gani wanafanya kwa watu wake. Si watu kulalamika, tulilalamika wakati wa wazungu, na sasa tulalamike hasa kwa nani. Lazima serikali ijue mtu aliye na watoto apate pesa kiasi fulani, sio elfu tano na mwingine yuko kule million moja.

Halafu vitu vingine President achaguliwe na party, party fulani ichaguwe President wa kutoka nje sio kwa bunge. Halafu yeye vile, vile, achaguwe Ministers kutoka nje, asichaguwe watu wa bunge, wabunge wawe wa unge, wa Ministers watoke kwa watu wale, wamefanya hapo zamani. Wawe experienced personnel, si wale wanachagua mbunge, kumbe yeye ni Minister, aweze kukaa vizuri.

Halafu vitu vingine kama AIDs, huyu mgonjwa wa AIDs sasa anatakiwa pengine hata Commisison waweke sheria, kama mtu anashika mwenyise kwa anamuambukiza rape, na anamabukiza yeye na AIDs lazima ashitakiwe kunyongwa kwa sababu amemuua.

Halafu maneno ya mimba ya wasichana wa shule, lazima wasichana wachunguzwe na hata hawa watu wafungwe, kwa sababu watoto wa shule siku hizi wanapata mimba hapa na pale, hakuna sheria, ndio hata wameleta ma chokora kwa barabara hapa. Asanti sana.

Com.Wanjiku: Asante Bwana, thank you very much bwana Kitiyo, na tunamuita Morris Kimogut.

Morris Kimogut: Basi Commissioners, mimi ni Morris Kurui Kimangut kwa majina na mimi nina machache ya kusema. Kwanza kabisa ningependa kusema ya kwamba, sisi tungependa tuende katika uchaguzi katika Katiba mpya. Kwa sababu nyinyi wenyewe ni wataalam wa mambo ya Katiba, mimi sitaki kusema ya kwamba pengine tufanye mwaka huu ama mwaka gani? Ni nyinyi wataalamu ndio mtakao sema, Katiba hii tutaimaliza lini? Na tutaifanya lini hata kama kwenda mwaka mmoja zaidi, ama miezi mitatu ama gapi si shida, shida tunataka Katiba ambayo inafaa wananchi wa Kenya.

Jambo la pili ambalo ningependa kusema, ni kwamba the Constitution of Kenya, the new Constitution should recognize the natives and their land. Kwa sababu hapa, ndio kumekuwa na matatizo, kwa sababu hata mmeona kama, the earlier Constitution kama inge-recognize natives and the native land hii problem ambayo mnaiona hapa, haingekuweko, lakini kwa sababu hai ku-recognize ndio shida hizi ziko na tumaini ya kwamba katika nyakati zingine this problem will not be there, and it is coming to an end today and for ever, it should not be there. Kwa hivyo utaona ya kwamba ninataka tuwe na natives, to recognize wao, kwa sababu ya nini? Kwa sababu hii ita-avoid grabbing, watu wanatoka sehemu mbali, mbali wanaenda Trans-nzoia ambayo haijulikani mtu wake, wana grabbe pengine nani anajua nyakati zingine they have people ambao wanataka power kutoka nje wanaweza kuja ku convince hata jamii fulani na kusema ya kwamba, citizenship yenu ni ya nchi fulani. Lakini nyinyi watu wa Kenya mtajitetea namna gani mtasema iko kwa Katiba, kama haki ya natives fulani iko kwa Katiba mtajitetea namna gani?

Ya mwisho ni kwamba hiyo italetu uhusiano bora kati ya makabila, tutajua ya kwamba mimi niko hapo, huyo ni upande ule, mwingine Nyanza, tutaheshimiana. Na hatutakuwa na mapigano ya kikabila, yatakwisha kabisa. Jambo la kufuatia ni kwamba tungependa tupate katika Trans-nzoia hii tungependa pia jamii ya ki Sabaot wapate representation katika Parliament na civic

wards, kwa sababu siasa ni kitu moja kigumu na hatari na inatakikana kila jamii iangaliwe unoana county kubwa katika Uganda, ina watu wachache sana, 17,00 voters, lakini serikali ya Uganda ilipotambua ya kwamba walikuwa tu jamii fulani ambao hawakuwa represented katika Parliament they were granted hiyo Parliamentary, privilege katika nchi kwa hivyo mimi naona ya kwamba kila makabila hasa katika Trans-nzoia hii yapewe nafasi after all we are Kenyans hakuna mtu ambaye ni wa nje. Kwa hivyo hata makabila yote yakipewa representation sioni shida yoyote, na jambo lingine la mwisho kwa sababu mnipigia kengere nataka niondoke sasa, nataka niseme hivi Commission hii haijakuwa fair kama wale wengine wamezungumza, na nitasema hivi kwa sababu mnaweza je kuchukua Commissioner kwenda kuwa chairperson katika sehemu ambayo kuwa chairperson kwa makabila ambayo wanazozana, hiyo inawezekana namna gani kwani Commissioner hawako wengi? Kwa hivyo mimi naona kama hiyo it is not very fair, kwa hivyo asanteni sana, na Mungu awabariki,

Com.Wanjiku: Excuse me Bwana Morris we did not understand your last point, what are you saying?

Morris: I said it is very unfair for this Commission to allocate duties, a Commissioner in an area where that Commissioner comes from, and they have conflicts with their brothers and sisters there, we should have a Commissioner from elsewhere, why particularly that group? Whom we are conflicting that is my complain. So, this Commission has not been fair at all to that effect,

Com.Wanjiku: I wanted to explain that which among is it among us,?

Morris:Not here but it wa in Endebbes area. Thank you very much.

Com.Wanjiku: Thank you, we take your complain. Can we have Nicholas Ngwanamu,

Nicholas Ngwanamu: Mimi kwa majina naitwa Nicholas Bwanamu Mungwana,nimekuja mbele yenu kuleta memorandum ya Kitale Jua Kali Artisans Association. Na nitaanza na yafuatayo, ndiyo niongeze yangu mbili kulingana na vile moyo wangu uko.

1. wana jua kali wamenituma on economy section. Jua Kali artisan request the Constitution Review to amend the law that will enable the economical mind to reach us in the country Kenya. so that taxation through licence to be controlled and loan interest to be low than that of KIE, which brings higher repayment to Jua Kali sector.
2. A law to be put in place to protect Jua Kali artisans from an warranted harassment usually planned by disatisfied well connected clients e.g on licences which is higher, which is on higher rate which they even do not harass Indians, but only on Jua Kali workers.
3. Inginge, a law to be amended in order distribution chain of raw materials used in Jua Kali sector is not controlled by only Indians from

Interjection Com.Wanjiku: can we listen to Mr.Bwanamwa please? Please let us give him a chance.

Bwanamwa: Tungelipenda sheria iwe hapo, itengenezwe isaidie wana wa Jua Kali Kenya nzima kwa ajili kuna watu ambao wanaingiza bidhaa hapa Kenya na tena wanasarisha tena wanauza na tena wanafanya hawking, hao hawaguswi kuhusiana na licence hata kidogo. Na wana Jua Kali wakijaribu kufanya kazi yao ya kutengeneza vitu vya ukarabati iwe kitu wauze, wanakuwa harassed na middlemen. Sheria itengenezwe isaidie hao, kwa sababu hiyo ndiyo njia moja ya kurudisha chini poverty

Halafu lingine upande wa economiy, the co-operative act to be changed and include also the law that can govern Jua Kalians to make up their co-operative. Kwa sababu ile law iko saa hizi, upande wa coperative inatawala chini sisi hatupati loan vile inatakikana.

Lingine upande wa economic tena tukienda kwa soko ya COMESA tuko na shida kuna mtu anaitwa middle man, ambaye kazi yake anakuja kutembea katika Jua Kali na ananua ile vitu imetengenezwa ambaye anapeleka kwa COMESA na anajigamba yeye ndiye ametengeneza kama kuna donors wale wanataka kusaidia ki kundi fulani inatengeneza vitu vizuri, unakuta huyo mtu wa middle ndio anapata vita vya Jua Kali kwa niamba ya Jua Kali na wale entrepreneurs wenyewe wanawachwa nje. Sasa mtusaidie law itusaide ili serikali ikifika mahali itusaidie sisi wenyewe tuwe tuna market huyovitu.

Kwa upande wa social kuishi watu wa Jua Kali, tungependa sheria itengenezwe watu wenye wanapanda miti kwa boma zao, sub-chief wanatu harass kwa upande kama wanataka kukata mti mmoja utengeneze kama jikoni, unataka kutengeneza labda kuni ya mama, unaona anataka ati permit. Maneno ya permit kwa upande ya miti ya individuals, hiyo iondolewe iwe tu kwa upande wa public in a forest.

Politica, upande wa Presidential powers, sisi watu wa Jua Kali tumesema irudishwe chini. Na upande wa Cattle rustlers, tunaomba mtu mwenye anapatikana na ng'ombe, serikali iweke sheria ng'ombe mmoja awe anafungwa miaka kumi na viboko ishirini, ili waogope kwa sababu hiyo ndio chakula moja ya watu wenye wanafanya kazi chini, chini.

Upande wa mama, yaani culture tutaomba serikali iweke sheria, isaidie watu wenye wanakuja kesho.

Interjection Com.Wanjiku: hiyo ndiyo ya mwisho?

Bwanamwa: Kwa sababu tuko na mavazi mengine ambayo zina wreck wanaume fikira zao na kufika mahali zinazalisha kitu inatwa ukimwi. Wa mama wapewe sheria ya ku dress in public kwa sababu wakati wanakuja mbele yako, wanavaa vizuri lakini ukitoka hapa nje tufanye home work mpaka line moja turudi, utashangaa vile wana tembelea kamisi badala ya nguo.

La mwisho tungeliomba kama kuna mashamba yanapeanwa, watu wa Jua Kali wapate plots, kila soko yote katika Kenya nzima ili azalishe kazi ndio poverty iishe.

Com.Wanjiku: Thank you very much Mr.Nicholas. Robinson Ngegu, I do not know if I am pronouncing it properly. Robinson so you will give us your name.

Robinson C. Ngeiywa: Mimi ni Bwana Robinson C. Ngeiywa, Nashukuru Tume hii kwa nafasi hii ambaye nimepewa, nina mambo kama manne hivi ambayo ninaka kuongea kwa ufupi.

Jambo la kwanza ni haki za watoto. Haki za watoto hapa nchini mara nyingi zimeguzwa maana ungeweza kuona watoto wa umri kati ya miaka nane mpaka miaka kumi hapo, wanafanyishwa kazi nzito, na waajiri wao pasipo kujali umri wao. So mimi ningelipendekeza kwamba hatua zichukuliwe kwa yule yeyote ambaye ataweza kutumikisha watoto wa kadiri miaka hiyo, kazi ya utumwa. Sheria iangaliwe vizuri inayo under watoto.

Jambo la pili kuhusu watoto hapa tuna watoto ambao ni mayatima, hawa watoto mara nyingi hawajapewa pia kusikia huru kama watoto wengine, maana mara mingi wao ndio wanatumiana kama watumwa ama kuajiriwa katika kuchunga ng'ombe au kwa njia zingine kufanya kazi katika nyumba kama maids. So ningependa serikali, au Tume hii ichukue nafasi hii na itunge sheria inayo weza kuwalinda watoto hawa, na hawa pia wajisikie kama watoto wengine. Wapewe haki sawa na watoto wengine. Mashule pia yaanizushwe na hawa watu wa council ya kuweza kutunza watoto mayatima, ili kwamba watoto hawa pia waweze kuona maisha mema baadaye.

Jambo lingine kuhusiana na wanawake, nitazungumza mambo mawili au matatu mahala hapa. Kumekuwa na msongamano wa wanawake karibu kila town na masoko, ambayo imelea shinda nyingi sana na kuna mambo ambayo yameudhi, hasa sisi kama wachungaji. Mambo ya prostitution yamekuwa juu sana. Unakwenda kuona kwamba wanawake hawa ukiuliza mume wako ako wapi? Hayuko lakini wamepangisha manyumba, na hii imeleta kusabazwa kwa ukimwi. So tunahitaji jambo hili liangaliwe kwa makini sana, kwa maan hata watoto wa umri wa miaka 12, 14, wamepotelea katika manyumba hiyo, za hawa wanawake, ambayo ni kinyume. Tunaka kwamba sheria iudwe kila mwanamke asiruhusiwe kupangisha nyumba kwenye soko bila mume.

Jambo lingine nataka kuongea kuhusu wanawake. Wanawake pia wapewe uhuru wao kama mwanamke. Mwanamke apewe uhuru wake kama mama, aheshimiwe na apewe haki zake. Kuna sehemu zingine wanawake wanagadamizwa, wanawake wanajuliwa kama kwamba si watu, lazima pia sheria itungwe ya kuweza kuwalinda wa mama, wengine wanadanganywa kwa muda kidogo na wanafukuzwa tena, halafu hawa wamezaa yeye watoto na hakuna mtu wa kutunza hawa watoto,

Interjection Com.Wanjiku: your last point Robinson

Robinson: Neno langu la mwisho ni kuhusiana na national dressing. Inahatajika pia kama taifa tuwe na national dressing, mavazi rasmi kwa wanawake, na pia ili kusudi kwa wazee pia, na hata wasichana au vijana, maana mavazi haya ambayo tunayaona sasa imechangia sana kwa mambo ya rape case. Wengine wanavaa kama kwamba wako uchi, na wanatembea na hii inavutia ina attract waume kiasi ya kutenda maovi, kwa hivyo ni vizuri sana waangalie mambo ya national dressing, hiyo itaweza kuleta discipline mzuri.

Mwisho ninaomba, kuna jambi moja tu ambayo ningetaka kuongea, mambo ya Police, force. Police force haijafanya kazi yake kwa njia iliyo nzuri maana wametumia mbinu mbali, mbali, za ku harass wananchi, na sheria ya Kenya inasema Police ni mtu wa kulinda amani. Lakini wamekiuka ile sheria na kugandamiza mwana nchi. Ndio tunaomba kwamba police wawe na nidhamu, na pia wanapoenda kukamata mtu lazima wapitie kwa mzee wa mtaa ili kwamba wafikie yule mtu wanayetaka akiwa na arrest warrant. Asante sana.

Com. Wanjiku Kabira: Asante sana Bwana Robinson, Bwana Robinson lakini kabla ya kuenda nikuulize swali tafadhali. Ningetaka kuuliza kwa sababu hawa wanawake wako kwa town, wako engaged na prostitution si kuna wanaume what are we going to do with those men? Kwa sababu huwezi kufanya prostitution peke yako.

Robinson: Nitasema kidogo, nitafafanua hapo kidogo ni kwa sababu ya kengele kunipigia ndio sababu ni sahau kutengeneza mahali hapo. Pia kuna wanaume wahuni pia ambayo mara mingi wamehusika kuvuja nyumba za watu wengine na pia wameendelea kuwapachika watoto wasichana mimba, na kisha kuwaachia mizigo, kwa upande wangu, ninaona kwamba sheria iwekwe ambayo kwamba ikiwa atampachika mtoto wa mtu mimba, au mwanafunzi, ni sharti alipe baba yake mahali, na kisha amchukue awe mke wake, kwa maana amemharibia ubikira wake, na pia akipatikana kama ameharibu nyumba ya mtu, lazima yeye alipe kama desturi ya sisi kama maasai, kama ungepatikana kwa mke wa mtu kama huyo mtu alilipa mali ng'ombe 30, ungelipa ng'ombe 30 na huyo mtu anabaki na mke wake, ili iwe adhabu kwake.

Com. Wanjiku: Asanti sana. Samson Ngoka, Samson go ahead.

Samson Ereka: Majina yangu naitwa Samson Ereka, mimi kwanza ningependa niseme kitu kulingana na mawazo yangu kwa upande wa haki ya msingi ya masomo. Nataka niseme hiyo kwa sababu tumekuwa tukidanganywa kila mara. Mwaka wa 1997, walitangaza hakuna malipo kwa watoto kwa shule za msingi, baada ya huo uchaguzi kuisha, malipo yaliendelea kama kawaida. Mwaka huu tumetangaziwa kwamba hakuna malipo kwa shule za msingi lakini nina hakika baada ya huu uchaguzi malipoyatakuwa kama kawaida, nimeona ya kwamba hakuna sheria ambayo imewekwa ya kudumu kwa hivyo mawazo yangu ni hivi, sheria iwekwe kwamba watoto wa shule za msingi wasome bure.

La pili kuhusu mali ya asili, kulingana na umri wangu vile nimetazama na kulingana na vile nimeona, nimeona ya kwamba kuna

wenyeji wanaumia, nikitoea mfano hapa Trans-nzoia nimeona, misitu nimeona National Park, nimeshuhudia na macho yangu miti ikikatwa ikielekea mahali pengine, na yule mtu ambaye alikuwa akiumia akichunga wanyama wasiharibu miti, wakipalilia, hakuna chochote, wamefaidikia. Kwa hivyo mawazo yangu nasema hivi, matoleo yeyote inapotolewa, kwa ajili ya national game ama miti kwisha kutolewa kusafirishwa, lazima mapato wagawie wenyeji wa hapo.

Lingine ni kuhusu makao, na kulingana na mawazo yangu na kufikiria kwangu, nimeona ya kwamba wakati Katiba ilipowekwa, wakaweka sheria ambayo iko Kenya hii, kwa Katiba ambayo iko sasa, inasema kwamba kila mtu anastahili kuishi popote katika Kenya. Niliona walipoandika, walipoandika ile Katiba, waliona ni vizuri sana. Lakini nimeona ya kwamba kulingana na mawazo yangu vile iliandikwa, haingiani na Kenya yote, inalenga tu mahali pamoja, nimeshuhudia Uasin Gishu, ukienda huko utaishi, ukija Trans-nzoia ukipata shamba, utaishi lakini nimekuwa kule Turkana sijawahi ona mtu yeyote akiishi huko. Nimeona ukambani sijawahi pitia Wafula kama amemiliki shamba huko. Na ukienda Kirinyaga sijawahi una Gema akiridhi huko imekuaje District hizi peke yake. Kwa hivyo nataka hiyo sheria iondolewe na mahali pake iwekwe sheria ya kila mkenya aheshimu, mipaka ile ya ma babu zetu wa zamani.

Basi nikimalizia nataka sheria ambaye inarenga watu ambao wanaleta mambo ya corruption, tumeshangaa mtu tunatangaziwa kwa radio mtu amekula mali yetu ya raia, ma milioni ya pesa na mpaka saa hizi, yeye bado anaendelea tu na kazi yake hajastakiwa hajafungwa bado anaendelea so tunataka sheria iwekwe ya mtu akipatikana amenyanyasa mali ya umma na afungwe. Asante.

Com.Wanjiku: Thank you very much Tony Korir, hayuko Tony Korir hayuko Damiano Odhiambo. Damiano Odhiambo.

Damiano Odhiambo: Asante sana Commissioner pamoja na wananchi ambao wamekuja kutoa maoni yao juu ya hii Commission yenu. Jina langu ninaitwa Damiano Odhiambo, mimi niko na maoni yangu mimi mwenyewe. Katika Trans-nzoia hapa, nilingia mwaka wa 54, wakati nilipo wacha shule. Na jambo ambalo nimekuja kusema hapa kwamba mbele yenu kwa sababu mmesema kushinda mimi, nyinyi ni watalamu mna ujuzi wa kila aina.

Jambo la kwanza ambalo ningeomba serikali yetu ambayo sasa imewatuma nyinyi hapa kwamba, watayarisha Katiba mpya ambayo kuna sheria ya kulinda nchi pamoja na wananchi wake. Jambo ambalo linanipa uchungu katika nchi yetu hii, ni hili. Sheria ilioko katika Katiba ndio ambayo itamlinda sasa, na hii sheria pia inalinda ma kampuni ambayo inaajili watoto wetu, na nikiangalia board katika Kenya ambayo ni ya Kitale hapa hakuna. Nikiangalia KCC ambayo ilikuwa inaandika wasichana, wetu hakuna. Na kuna sheria ambaye inarida hizi ma board zote. Ndio ningeuliza nyinyi Commissioner katika hii Katiba ambayo mnaitengeneza mpya muweke maanani zile sheria za kuweka nani katika hizo board ili isiwe tena aibu ambayo tunaiona wakati huu. Ni aibu kwa serikali, ni aibu. Ikiwa watoto wetu hawana kazi, board ilikuwa hapa imebeba watu wengi, siku hizi haikuna, KCC ilikuwa imebeba watu wengi, siku hizi hakuna. Nikirudi katika upande wa Kenya, katika Kenya, Mungu alitweka makabila 42. Na haya katika makabila 42 Mungu alijua kwamba haya makabila wataishi katika Kenya

wakiwa kitu kimoja. Kwa hivyo ni heli wawe wakijua kwamba Mungu anawapenda, ili waishi katika Kenya kama kabila moja ambalo ni kabila 42, Mungu amewaweka kama vidole hivi vitano, lakini wanafanya kazi pamoja. Tafadhali mfanye kazi pamoja kama vile Mungu ametupa Kenya.

Nikiwacha upande wangu wa maoni yangu juu ya watoto wetu. Serikali yetu wakati walipokuwa wakisema kwamba watoto watakua wakisoma bure, pale shule ya msingi wakati huu tunao watoto nyumbani, hawaendi shuleni, kwa sababu kuna pesa ambazo zinatakiwa shuleni na hali serikali yetu, ambayo inatushinda ilisema kwamba watoto watasoma bure, kweli hii tunaelekea wapi, huu ni upendo ambao Mungu alisema? Mungu awabariki.

Com.Wanjiku: Thank you asante mzee Damiano, thank you very much. Erick Korot

Erick Kolot: Majina yangu ni Erick Chesiro Korot. Ningependekeza maoni haya katika Tume ili kwanza, Katiba ni lazima iandikwe katika lugha ambayo naweza kueleweka na mwananchi wa kawaida.

Jambo la pili, democracia. Democracia Kenya ni ya watu wengi, lakini watu wachache Kabila ndogo linaumia, kwa nini niseme hivyo. Uchaguzi ambao tunaambiwa ya kwamba majority votes lakini minority votes lakini minority votes wanakosa kuwa na mwakilishi wao katika bunge. Ningependekeza hivi, kabila ndogo katika Kenya ni lazima wapatiwe special seats na Constituencies inaweza kuongezwa. Jambo la kufuata ni ya kwamba, wewe kama mgombea kiti wa bunge, ni lazima uende bunge katika muda wa three terms. Ikipita hapo ikizidi hapo, wewe u retire uachie wengine.

Jambo la kufuata ni Presidential powers iweze kupunguzwa. La kufuata pia ni ya kwamba mawaziri ambayo wanachaguliwa katika mawizara mbali, mbali wawe na taaluma. Jambo pia la kufuata ni ya kwamba jinsi ambavyo tulipigania uhuru, tulipigania uhuru kutoa upumbavu, umaskini na magonjwa. Lakini kufikia sasa ni mwaka wa 40 tangu tumepata uhuru tunaona umaskini bado upo, magojwa yapo, na ujinga umezidi. Pendekezo langu ni hili; Umasikini kwa sababu umezidi kwa watu wengi, serikali ingeona jinsi ya kusaidia hawo watu kuwapatia pesa kidogo, kidogo ya kuweza kufanya biashara hapa na pale.

Kuhusu ujinga, ningependekeza ya kwamba watoto wote, wasome bure, iwe ni shule ya msingi, shule ya upili wasome bure. Kwa sababu Kenya ni nchi tajiri tukiweza kukaa vizuri, tunaweza kufunza watoto bure. Upande wa magonjwa, magojwa pia yawe bure matibabu tupatiwe bure let us enjoy the privileges of our country because we fought for independence. Na pia la kufuata Bwana Commissioner ni ya kwamba Tume nyingi sana zimekuwa zingibuniwa lakini hatuoni matunda yake, hatujui pia ya Ghai itavuna matunda? Ni hayo tu Mungu awabariki, asanteni.

Com.Wanjiku: Thank you very much, thank you bwana Erick. Nicholas Kiboi, Nicholas Kiboi hayuko akiwa hayuko tutamuita William Khaemba.

William Khaemba: Mimi ni William Khaemba Sikenga. Mimi ni mkaazi wa Trans-nzoia nimekwisha kuwa mzee hapa, leo watu wanakuja na maneno mengi sijui wanataka kubomoa, sijui wanataka tufanye nini? Mimi naleta maoni yangu Kenya wakati tuliopata uhuru tukafanya Katiba ile ilikwisha tulikuwa watu karibu million 7, namna hii ndio tukaelekea karibu 9. Na mashamba yalikuwa mengi kwa sababu mzungu alikuwa anahama wengi wanataka wanataka mashamba yao, lakini yaliuzwa. Na kama walinunua wewe utatoa mtu huyu? Mpe pesa. Kitu ambayo kiko atika Katiba ya leo mimi nilikuwako kwa ile Katiba inahusika hii, nilikuwa ndani, mimi nafikiria namna hii, watu ni wengi wamekwisha kuwa wengi, na watu wengine tusikumbuke hapa Kitale peke yake, Trans-nzoia, tukumbuke Kenya mzima. Watu wengine wana mashamba zaidi ya acre 60, mtu mmoja anafungia kuku, nyoka inatembea ndani na mwingine anatembea bure hana hata kidogo hata mahali pa kulala. Mimi nafikiria bunge la tisa ambalo linakuja jipya lile, liende likae libadulushe mkondo, lifanye mtu akiwa anataka kubakia na shamba lake, ikiwa ni acre zaidi abaki na acre 500 ingine wapatie maskini. Kwa sababu squatter, Mzungu alienda na akawacha watu, bado wanaoitwa squatters wako hapo, tuwaita squatter mpaka miak gapi? Hii tutakuwa tunaenda mbele au tunarudi nyuma. Ni lazima muweke hiyo kwa Katiba, ambayo nyinyi mnaandika. Mambo yale wanasema ninasikia watu wanasema Katiba mambo ya miti. Unajua wakati mzungu alikuwa anaenda, aliwacha miti nchi hii mingi sana, lakini watu wakaja wakakata miti hiyo wakamaliza, mvua ikakosekana. Kwa hivyo sheria iwekwe iwe kwa Katiba ile, watu wasikate miti bure. Kwa sababu miti ukikosekana, tutakosa muva na njaa itakuwa Kenya.

Mambo ya President, tukiwa tunataka tuwe na President lazima President awe na mamlaka. Kwa sababu niseme hiyo, nchi ya Africa inafikia mahali fulani watu wenyewe wanakosa ukweli wanaharibu serikali. Kwa hivyo President awe na uwezo akichagua Prime Minister achaguwe na mawaziri wake. Uwezo huo usitoke, President abaki nao. Kwa hivyo kwa sababu saa ni mbaya, mimi nasema namna hii, bwana Commissioner kama muko hapa, watu wamekwisha zungunza maneno ya wajumbe, mjumbe akienda sisi tulipiga kura, wacha yeye akule atatoka atarudi, ndio tuangalie maneno yake lakini bure tusizungumze.

Mimi ninasema namna hii Katiba ya mashamba tu mashamba hiyo irekebishwe mwe nayo muweke kwa kifungu, iwe kifungu number fulani, na iwe inasaidia maskini, ugonjwa wa ukimwi, weka ndani kwa sababu ugonjwa huu umekwishamaliza watu. Kwa hivyo mwenye kengele amepiga lazima nimheshimu. Kwa hivyo hapo, mimi nimefikia hapo, asante.

Com.Wanjiku: Asante Bwana Khaemba, Honourable, honourable Moiben,

Hon.Samuel Kisilo Moiben: Thank you very much Commissioners, yangu ni mafupi ningetaka kuanza hivi, katika Kenya Katiba ieleze kwamba mtu ambaye anataka kiti ya siasa iwe ni ya councilor, Parliamentary ama u President aende three terms. Majina yangu ni Samuel Kisoro Moiben. Parliamentary hata kama mtu ni kama malaika, three terms aende nyumbani, councilor hata kama ni mzuri namna gani, three terms. Na niseme hivi watu wamesema mengi mambo ya gender. Kweli mimi ni mzee niko na miaka 55, ukitakata kuachana na bibi yako achaguliwe kuwa councillor, utatafuta bibi mwingine. It is experienced because I do not know what happens Commissioners with all due respect madam, our gender, the weaker sex as soon as they are made bosses, they mistake for freedom the other way round, and they begin misbehaving. So kweli tunapenda nyinyi sana

wa mama na tunataka kusema kwamba tuheshimiane hata ndio nimesimama sababu ki mila yangu inaruhusu wanaume wasimame wakiongea, wamama ndio wanakaa, sababu anaweza kuwa na mzigo. Tukiendelea Commissioners, kweli katika Kenya, tuna makabila mengi sana, mimi nilihesabu ni karibu 70, kusema makabila ni 42 ni uongo makabila ni 70 napendekeza kwamba, Bunge la Kenya ligawiwe mara mbili, upper house iwe ndio kila kabila katika Kenya iwe na mtu wao mmoja, kila kabila whether kubwa, ndogo, iwe na mtu mmoja kule wa kusikia mambo yao, sababu niwaambie unaweza kosa meno yote kwa mdomo na unaishi, lakini ukikosa ulimi, umekufa. Kwa hivyo tunataka kabisa ulimi ufanye kazi. Kama huu mkatano tunatumia sana ulimi, na baadaye tutamia meno jioni siyo, kwa hivyo nafasi ya utawala huenda sambamba, na ulimi, tutukuze Mungu kufanya haki kwa kila kabila. Tukija chini tunasema kwamba maneno ya umaskini, nina pendekeza kwamba, mtu aliye maskini kabisa katika Kenya awe na aridhi acre kumi, anayeweza kuwa na zaidi lakini isipite 300 sababu ikipita 300 ananza kuwa na pembe.

Masomo ya primary mpaka secondary yawe free, katika Kenya. Lngine ambayo napendekeza ni kwamba ugonjwa kwa kweli watu wote wanakufa sana hii maneno ya cost sharing kwa hospitali haina maana hata kidogo. Sababu hizo pesa mara nyingi zinaimbiwa. Hata unaweza soma kwa gazette kesi ya Kenyatta ni nani director yuko ndani, ma millions anashtakiwa sababu hiyo premature case siwezi sema mengi. Hiyo ni mfano tu lakini chini, chini huko cost sharing ipigwe marufuku, watu wapate dawa free. Nikiendelea ningesema kwamba katika nchi yetu jirani ya Uganda ni nusu ya Kenya na watu wa Uganda, ni watu million 15, sisi tuko millions 30 lakini Commissioners, Uganda iko na MPs 300 sisi kwa hilo ujue tuko na tambia mbaya tuko na 210, ningependekeza kwamba Kenya inaweza kuwa na MPs bila wasi, wasi, katika lower house ili watoto wa watu wapate kazi, 400 we can afford 400 MPs na kila kabila inafanya kazi yake, ili tusiwe na wasi wasi.

Nikimalizia Commissioners, ni kwamba napendekeza serikali ya majimbo. Majimbo ili kwamba hizi Wilaya mipaka yao itolewe, ibaki tu ya Province. Ili Province hasa kama Rift Valley iwe ni states 3, North Rift state, Central State, na Maasai state huko chini, halafu ingine sasa kama Western ni Western state, Nyanza namna hiyo, ili kwamba hawa councilors, kunaweza kuwa na Mayor hapa na Local authority lakini ya county council iwe ma District nne wachaguwe chairman wao, ambayo anaitwa Administrative secretary. Hii maneno ya authorities sana sana kama ambaye tunayo sasa, ni wizi mtupu. Pese za LATF wanakula pesa za LATF hata haoni hata pipes, wanakula pesa za maji, na ningependekeza maji hata kama ni ya Municipality, yachukuliwe na wizara, Ministry of water, ifanye Kenya nzima mambo ya maji na tena Ministry of Agriculture, na Ministry of forestry wapande miti barabara zote za Kenya na ndizi wakitumia mabusu ili watu wa Kenya wakitembea na miguu wanakula na kuna kivuli. Nikimalizia Commissioners, tunawashukuru sana tunawaomba nyinyi sana, mfanye haki kwa watu wa Kenya hii, maneno ya extremism mtu mwingine kuwa extreme kwa makabila ingine, Mungu atuumba sisi wote, aliuumba kabila kubwa na kabila ndogo, heri tufanye haki, "kikulacho kinguoni mwako" aliyekuwa anashtaki marehemu Kenyatta alikuwa ni mkikuyu unajua Macharia, aliyepiga risasi Yitzak Rabin ni myahudi, aliyemsaliti yesu ni Judas, tufanye haki. Asanteni sana Commissioners.

Com. Wanjiku: Asante sana, tafadhali mheshimiwa, Martin Musambi.

Martin Musambi: Asante Bwana Commissioners kitu ambacho naenda kuongea, kwa maoni yangu inahusu vitu ambavyo sitaki kusahau, wanawake na wanaume, haki ya mtoto, majina naitwa Martin Musambi mkaazi wa Kitale hapa.

Tatu utamaduni, nitaanzia kwa watoto na lazima mtoto apewe haki ya kutosha, Tume inasema ya kwamba mtoto lazima ahakikishwe kwamba anasoma, anakula vizuri, anakunywa vizuri analala vizuri, anavaa vizuri. Na upande mwingine tumemkosea, tumewakosea watoto hawa tumewanyima haki moja, mtoto anavyoenda shuleni, ananyimwa kiboko, na mtoto asipochapwa kiboko huyo mtoto hatarekebika, mtoto lazima ahukumike hata Bibilia inatuezeza ya kwamba mtoto usimnyime kiboko, mara ya kwanza, hapo awali zamani watoto walikuwa wananidhamu, wenye nidhamu kwa wazazi, walikuwa na nidhamu kwa wazee, walikuwa na nidhamu kwa serikali hata na waalimu, lakini saa hizi watoto wamemea pembe, kwa sababu unapojaribu kumchapa kiboko anasema si walitangaza sisi watoto tuko na haki kwa sababu hatuwezi kupewa kiboko. President alichapwa kiboko, waziri alichapwa kiboko, baba alichapwa kiboko, hata mwalimu alichapwa kiboko, hata Commissioner walichapwa kiboko, kwa hivyo saa hizi, inatakikana mtoto achapwe kulingana na nidhamu si tuwachape kwa kimakosa, lazima mtoto huyu asipochapwa kwa kiboko, kuna wengine wamemema pembe wanafanya kazi chaos, kuna wengine wanafuta sigara, kuna wengine wanakunywa pombea kwa sababu hawataki kiboko, wako tu na nidhamu ya kusema mimi nikichapwa kiboko huyu mwalimu atashatakiwa, hata mzazi akimkuta baba wewe unanda wapi? Anasema wewe wacha mzee, kwa sababu hawana nidhamu.

Uzao wa wanawake nao, na wanaume kulingana na Bibilia inasema ya kwamba na nilazima mwanamke awe chini ya mume wake. Mwanamke akiwa na masomo ya kutosha ni lazima aajiliwe, mwanamke anatakikana afanye kokote anakohitaji kama anaweza, lakini tukisema ya kwamba mwanamke awe sawa na mwanamume, hiyo italeti mafarakano na heshima haitakuwako. Kulingana na sheria ya Bibi inasema ya kwamba, uwezo wa mwanadamu uko kwa mwanamume sio mwanamke, na lakini sisi hata wanaume, lazima tuwapende wake zetu, kulingana na bibilia vile inavyosema. Tusiangalie maneno ya ngambo peke yake, na nilazima tungalie mambo ya Africa. Unapoangalia sana vitu vingi tunangalia huko, kwa uingereza peke yake lakini huko hatuungalii. Nasema hivyo tukiwa na usawa ndani ya nyumba, mwanamke huta mkosoa, ukimkosoa anasema hata mimi naenda, kwa sababu mwanamke huyu atasema hata wewe ukitaka hata mimi naweza kwenda nipatiwe urdhi kwa sababu hana nidhamu, na hiyo haitakuwa na heshima, pili heshima haitakuwako na talaka itapatikana, ukahaba utapatikana.

La mwisho lazima mavazi iwe ya kupendeza ya kisawasa, ya nidhamu, si vilei mwanamke anatembea, anatembea uchi, askari akiwa kwa uniform anatakikan aende kwa field, sasa inaonekana ya kwamba, mwanamke akitembea hivyo anajulisha wanaume ya kwamba yeye ako huru kukabiliana na mwanamume. Asante.

Com.Wanjiku: Asante sana, can we plead with you please to keep quite, and when you are walking out ujaribu kukimia kwa sababu tunataka kusikiza kila neno la kila mtu, na tunafanya recording na tunaona kama recording iko hapa, na it is only recording only the noise. So I think let us try to be careful asenteni huyo alikwa Harun Keboi, Harun Keboi halafu atafuatwa na

Harun Kemboi: Asante, Mr. Commissioner sir, it is my high chance to have reached today Lancaster house. Mr. Commissioner, my name is Harun Kemboi Khaemba. Mimi ni Mluhya, na nilizaliwa kwa ADC ya Olgadongo, baba yangu anaishi ADC, mimi pia nimekuja kuishi ADC. Sasa maoni yangu leo ni wakati nilipokuja hapa mara ya kwanza milioni watu wakila mori wakisema nchi yetu, nchi yetu. Na nimefikia kiwango ambapo ningependelea, niseme hivi, nitarudi mpka kwa wazazi wangu, niwaulize ikiwa kweli hii nchi ni ya wanyewe, inabidi turudishwe sisi wengine tunaweza kubali twende, kuliko tuuane.

La pili lazima tuheshimu utamaduni wa kila kabila kwa sababu watu wengi wamesungumzia ya kwamba, sisi tuko na nchi yetu sasa hapa tunaishi kwa nchi yetu tunanyanyaswa kwa nchi yetu, I am sorry to say so. Nimeona councilor Muliro amezungumza hapa kama mama mkongwe and she is a Kenyan by citizen lakini, yeye anatoka South Afrika. Yeye anaweza kuwa anaelewa zaidi, yeye anaweza kuwa anaelewa the deepness anaweza kuwa anaelewa zaidi kuliko mimi. Sasa maoni yangu ni haya, ikiwa ni haki Commissioner ya kwamba sisi tulitoka Uganda, turudishwe, kuanzia leo.

Ya pili kuhusu, nitazungumzia kuhusu Judiciary. On the side of Judiciary madam, ama Commissioner, ningependelea all courts, all judges kwanza, itengenezwe huko nyubani kabla ya kufishwa kwa kortini. Ya mwisho mzee Commissioner. Wacha nitoke basi.

Com. Wanjiku: Excuse me tutamuuliza mtu akiwa anazungumza asitumie majina ya watu, si ndiyo, so let us not mention people's names peana tu pendekezo lako, lakini usitumie majina ya watu. Asante Joseph Chemaswet, Joseph ako? Hayuko kwa hivyo Joseph Chemaswet hayuko. Noah Bet.

Noah Bet: Wana Commissioner, na wazungumzaji wote, imekuwa masikitiko kwangu maana nimeona Sabaot na wa Bukusu peke yao wakizungumza na sisi ni waakirishi wa kabila zingine kama wa nandi, na nimeona

Interjection Com. Wanjiku: Tafadhali mumuache, wakati ni wake.

Noah: Maana ni mtu wa pili maoni yangu ni hivi sioni vibaya yale maoni nyinyi mmetoa vile imesemwa tumenyanyaswa, hakuna kunyanyaswa, sisi ambao tulikuja, hatukuja kulazimishwa, maoni yangu ni hivi, Rift Valley ikae mara tatu, iwe North Rift, South Rift na Central. Na serikali ikae kama vile tulikuwa tunakaa yani kama PC atakuwa kama kawaida. La pili kwa jina inaunga pamoja, tuweke Kitale, iwe na Kitale sio maneno mbaya. Iwe jina la kale na itakuwa Kitale ya kila mtu si Kitale ya Sabaot peke yake. Kama yako mashamba tutapatia waSabaot hakuna ubaya wazee, kama bado yako mashamba yetu sisi tuwapatie. Ya mwisho Kenya tuwe watu wa kuzaa watoto kama tano, mwisho, iwe sheria. Maana nimeona Kenya tutakuwa squatter maisha na maisha maana yake mtu huzaa watoto kumi kesho anasema hakuna shamba, kwa hivyo naomba kwa

kuweka sheria, mtu akizaa watoto 1-5 iwe ya mwisho na hiyo ni yangu sina maneno mengine.

Com.Wanjiku. Asante sana, they are so excited what do we do? Can we plead with you again, to keep quiet so that we can have a better recording. Tafadhali asante, Ben Kiso, Ben Kiso, wewe ndio Ben.

Ben Kisos: Kanyenuuani kekureno kamache ng'alale ng'ale kaab walemanik.

Translator: For you Commissioners angetenda kuzungumzia mambo ya walemavu.

Ben Kisos: Kasate kule kunyor ngichek walemanikboichoisiet kuchakee ng'way akoe

Translator: angetendekeza kwamba walemavu pia wapate uongozi, wapate kupewa nafasi ya kuongoza kuanzia chini mpaka juu.

Ben Kisos: Kito ake kokochi kunyor serikali walemanik lawyer ambu kila District nyi jongine.

Translator: Walemavu mara nyingi huwa wanasahuliwa na watu wengine kwamba sio watu, kwa hivyo angetendekeza pia wapewe lawyers kwa kila District at least ya ku represent ama kusimamia wa walemavu.

Ben Kisos: Kito ake nyateshine lekokaab walemanik kenyaru mbo tibik sikyinee chito nyi mzima lekwet aki moti yoo. Kunyo keuundan sheria chiribo

Translator: amesema mara nyingi, kuna wasichana walemavu na watu wengine huwa wanawapatia mimba na kuwaacha hapo, kwa hivyo anasema hiyo sheria itengenezwe ya kuchunga hawa walemavu.

Ben Kisos: Kaamache ang'alale ng'alekaab kamutusijiet

Translator: Anataka kuzungumzia mambo ya kuoa.

Ben Kisos: Miite biiko alake chi mute lekokaab angukwat.

Translator: kuna watu wengi sana wanaoa wasichana wa watu wengine na kuwachia hapo baada ya kuwapatia mzigo.

Ben Kisos: Meche sheria keecha nyikaaram nyimuche kirib biiko.

Translator: Kwa hivyo sheria lazima iundwe ya kuwadhibu hawa watu.

Ben Kisos: Ng'alekaab kaleksiet imuche kolachekei koruk miatya nto niyo katiny chitake muchasta ngeraat chiito mochoktoos kekas kule kelach kei chitiito kunee

Translator: Ile amesema mavazi sana wanawake wanavaa vazi lile baya halafu baadae mume anaweza kumrape ama kumnyemelea halafu tena baadaye yule mtu ambaye amenyemelea kwa sababu ya mavazi mabaya huyo mtu anashikwa na kumbe chanzo ni yule mtu ambaye amevaa vibaya.

Ben Kisos: Yemekei kule korko ake tukui nyi mii Kenya kunyor santenyi.

Translator: amesema kila mke ambaye ako Kenya apate mume. Asante.

Interjection Com.Wanjiku: Kila mke apate mume

Translator: amesema ya Commissioners, kila mwanamke ambaye yuko Kenya apate mume ama bwana.

Com.Wanjiku: Wycliffe Barasaza. Wycliffe Baraza.

Wycliffe Baraza: Kwa majina yangu naitwa Wycliffe Baraza, ni mkaazi wa Trans-nzoia. Mimi nataka tu kuongea maneno mawili, matatu hivi. Tangu uhuru tumeweza kuwa tukisema kwamba tutaondoa umaskini, lakini hadi sasa bado tunaita umaskini mimi napendekeza jambo moja, utapata familia moja katika Kenya mwisho wa mwezi haiwezi kupata hata shilingi moja, na utapata famili nyingine mwisho wa mwezi, inapata shilingi 200,000. Hivyo inaendelea kuweka ile gap ya maskini na tajiri, hiyo gap haiwezi kuisha. Ningelipendekeza hivi, sheria iundwe kwamba, wewe ukiwa unafanya kazi fulani na wewe labda ni Executive katika ile kazi, familia yako iwe ni moja tu, haijapatikana ikifanya hiyo. Kwa sababu iwapo wewe utakuwa mkuu wa jeshi ama labda tuseme wewe ni mkuu wa shirika fulani, utapata mwanamke wako anasimamia shirika hilo labda sehemu nyingine. Mwana mtoto wako, pia atakuwa katika like shirika yaani nyinyi peke yenu mmezaliwa kupata kazi katika lile shirika, ili hali watu wengine wote wamesoma.

Hivyo sheria iwekwe, sheria iwekwe kwamba kazi ikiwa ni moja, labda mtu kutoka familia hiyo iwe ni watu wawiwili, wakizidi watu wawili wasizidi watu wawili kufanya katika lile shirika. Pia iwe kwamba iwekwe sheria kwamba, kazi inapotokea ama familia hiyo inapopata ujira wake mwisho wa mwezi, familia hii ingine nayo pia ipate ujira, iwe kwamba, wewe vile unapata huyo anapata. Upande wa pili, ni upande wa jeshi, mimi napendekeza hivi, askari wetu ama jeshi letu haswa linapata mshahara bila kazi. Napendekeza iwe ni sheria ya kwamba kazi kama za ujenzi wa barabara, kazi kama kutengeneza ma hospitali badala ya kuleta watalaam na serikali kuwapa contract waje wafanye hiyo kazi, jeshi letu, lichukue mamlaka ifanye kazi, pesa zibaki katika taifa lenyewe.

Kwa kumalizia upande wa silaha, ningelipendekeza sheria iweke sheria katika silaha iwe ni kwamba, jeshi peke yake inaruhusiwa kukuguzwa bunduki. Bunduki iwe ni sheria kwamba mtu mwingine yeyote asije akapatikana na bunduki hata akiwa ni Minister, bunduki iwe ni kwa yule mtu ambaye ni mtaalamu wa bunduki na awe ni mwana jeshi. Sababu hata hawa hii mabunduki kupatikana kioyo ovyo, inafanya uhalifu wa bunduki unazidi kuwa mwingi, hivyo hayo ni yangu machache.

Com.Wanjiku: Asanti sana Bwana Baraza. Gabriel Mangoli,

Gabriel Mangori: Kabla sijasema kitu, nitaomba Mungu anisaidie niseme maneno ya kuweza kujenga Kenya yetu maana mimi ni mzee. Asante kwa majina ni Gabriel Mangoli.

Kitu cha kwanza sitasema maneno mengi nitasema kama mimi ni mwenyewe. Kitu cha kwanza, ma-officer wale mmekuja, ninataka mkipenda ikiwa ni haki serikali ya Kenya imewatuma nyinyi kuja kutembelea hawa wananchi, kuchukua maoni, nikiwemo mimi. Nina wasihi kwa unyenyekevu kwa heshima yenu, chukueni hili jina squatter litoke Kenya. Jina squatter litoke Kenya, shida nyingi Bwana Commissioner ama ma-officer wale mmekuja, ugonjwa mwingi, hata mnasema ukimwi umekuja nini imekuja mama akikosa shamba, na mtu apatikane wa ukimwi atakosa kupata hiyo ukimwi wananchi. Mimi sitakusumbua kwa maneno mingi hata hutaona nikipigiwa kelele. Ninaomba tu kwa unyenyekevu kama ni haki serikali yetu ya Kenya ambayo inongozwa na mzee Moi imewatuma, tafadhali squatter, jina hili litoke kabisa. Wakati mimi nilizaliwa hapa labda wengine wanakudanganya, mimi nilizaliwa hapa, hata baba yangu alikuwa Magistrate, zamani walikuwa wanasema President zamani, nilizaliwa hapa, na sitaki kujisifu, mimi ninaonge kwa watu wa Kenya hapana kabila ya Kenya ya ukoo hapana, nasema kwa watu wa Kenya nzima hata Mombasa kitu squatter itoke. So ninaomba kwa unyenyekevu jina squatter ikitoka watu wapewe mashamba, na isiwe style hii inafanywa, shamba linapopatikana, linapatikana na ma-officer wa serikali wanasema shamba limepatikana tayari hilo shamba linauzwa. Jee Commissioneer tutasema nini mnataka tufanye nini? au umaskini ule serikali inasema inataka kupunguza umaskini, itafanya njia gani? Kitu tu mimi ninasema wananchi wapewe mashamba na isiwe ati squatter au nini hata nikisema hivi matajiri wale walipata ndio bado wanaendelea, asante sana.

Com.Wanjiku: Asant sana Bwana Gabriel Mr. Richard Situma, Richard hayuko, Eliud Nabiba.

Eliud Nabimba: My names are Eliud Nabimba I would like to present my own opinion as follows:

1. In the new Constitution, there must be a maximum number of political parties in Kenya, I propose two.
2. There be put an age limit and the term limit for Members of Parliament and councilor, I propose seventy years and three terms respectively.
3. The President must be above party and Constituency politics and should have also three terms of service, five years to remain as one term.
4. Councilors should have at least a basic minimum education level of form four, with D+ and so to the Mayors and

chairman of local authorities.

5. Mayor should be elected by voters directly for them to appoint deputies and chairmen of the respective committees and so to the chairmen.
6. Duties of an MP should be stipulated in the law and the outline of their work, be known to the voters to avoid confusion.
7. There should be a maximum possession of land in terms of hectares. I propose a 100 hectares of land.
8. Industrial court should have branches in all Provinces, if not in all Districts.
9. Special seats in Parliament should be preserved to worker i.e Unionisable women, youth and disabled. I propose five in Parliament and at least one or two in all Local authorities and all those be made Ministers to be led by them.
10. There must be an industrial court of appeal, Chief Justice be appointed by Parliament and him or her to appoint Judges of High Court and courts of appeal. Judges of the Industrial court must be approved by Parliament.
11. The number of Ministries be determined by Parliament and not the President. Thank you very much.

Com.Nunow: Thank you, please you could register yourself, then we Joseph Wasilwa, ajitayarishe Lazaros Wangwe.

Joseph Wasilwa: Basi ni mimi ma Commissioner wote na wananchi wa Trans-nzoia, langu ni kwamba mimi ni Joseph W.Wasilwa. Kwa ajili ya Trans-nzoia, ya kwamba wa koloni wametajwa wa koloni walisukuma watu kwenda mbali, makosa hiyo ilifanywa na wa koloni na serikali ilikuwako ya Kenyatta, huenda labda tuhitaji maktaba yao tujuwe ukweli uko wapi, kuna mzee mmoja amesema pale ya kwamba tukae chini kwa amani, sisi na wa Sabaot tumeoana hawo ni wajomba, nini na nini hatutaki lolote lile la hasira, kwa sababu hasira huaa na haibebi, kwa hivyo tunahitaji ya kwamba labda kama makosa ilifanywa na watu wa mbele hatujui kwa sababu wengine walisema ya kwamba hawakukuwa na viongozi. Kwa hivyo wacha itengenezwe kwa sababu hii sheria iko. Yangu sina mengi.

Com.Nunow: Asante sana Wangwe Lazarus ajitayarishe John Kapkwon.

Lazaros Wangwe: Mimi kwa majina na Lazarus Wangwe, niko na machache sana ya kusema, la kwanza ni la kuhusu mashamba. Hapa Trans-nzoia pendekezo langu ni mtu aruhusiwe kukaa pahali popote kufuatana na uwezo wake na aishi na enough protection kutoka kwa serikali.

Kuhusu elimu ningependekeza ya kwamba, wale walemavu wote, wapewe free education upto University level if possible. Electoral Commission ningependekeza, ipeane kwa President, terms mbili na kwa Parliamentary seat pia iwe terms mbili, na civic terms tatu. Na pendekezo lingine linakuja, kufuatana kuongezea tu kwa maoni yangu, napendekeza ya kwamba hapa Kenya watoto wapewe elimu ambayo itahusisha elementary law, ili watoto wakue wakijua mabaya na mazuri kufuatana na the rule of law. Zaidi ya hayo kufuatana na maoni yangu, mimi naona Kenya ni tajiri sana, lakini pesa nyingi inawekwa nje, na ninapendekeza pesa zote hata zikiwa za President ziwe banked hapa nchini.

Nikimalizia ningependekeza kwa Provincial Administration, kwa sababu tunataka watu waishi na roho njema kila pahali, Provincial Administration, Chiefs na assistant chiefs na hata mkasa, wao wachaguliwe na raia asanteni.

Com.Nunow: John Kapkwon, Miriam Nabuja ajitayarishe.

John Kapkwon: Commissioners jina langu ni John Kapkwon Mjapara, nina machache I will start from Presidency. Mimi nina maoni kwamba,

1. The President should not be an MP. He should be elected directly by the majority of Kenyans.
2. Appointments as regard the Cabine, the Cabinet kwanza iwe very small
3. It should be on merit sababu, I have not been very impressed as regards some of the appointments unatoa mtu pengine mtu wa form four na sababu ameenda Bunge you take him to be the Minister of health, what does he know about health? Mimi naonelea ya kwamba there Ministries which need people who have the qualification, kama Ministry of health you must have a Doctor, kama ni Ministry of Industry you must have an Engeneer something like that,
4. Vikijua within the local area, all the resources sema kama ma forest, game parks, maji, should benefit the local people by literal say, 50% should go to the development of the locas.
5. Kitu ingine we have also the problem of the currency, sema pesa ya Kenya. From the beginning we had mpaka Independence tukapata pesa, na tukaweka kichwa ya mzee Kenyatta when he went tumekuwa na current President kichwa yake iko kwa notes, so when he goes this year or next year, mimi ninajua ya kwamba ku print hiyo pesa it takes a lot of foreign currency. Mimi ningenelea we put either map ya Kenya, na crown iwe juu ya pesa yetu, so that whichever comes hiyo noti inaendelea always.
6. Kitu ingine mimi, ninaonelea pia once you are touched as corrupt in one way or the other mimi naona kama katika nchi za nje, when somebody is touched kwamba he has committed an offence somewhere, he has to resign, because I have seen of recent now you find somebody has very big case in court he has embezzled several millions of shillings but anaendelea kukuwa Minister, anaendelea kuwa Director, hiyo mimi naonelea that is abuse of powers, asanteni.

Com.Nunow: Asante sana, tafadhali wale wanajitayarisha kutoa maoni muweke point zenu at least point tatu nne straight you to those points because we have reduced the time from five minutes to three minutes and three minutes you can say upto to 10 points if you are well organized, so that we cover as many people as we can. If Miriam Nabuja is not there, I can see her then Julius Laibich

Julius Laibich: Thank you Mr. Commissioners, Ladies and Gentlemen, I only have few points I want to present, my names are Julius Shedick Laibich.

Leadership: There should be a federal system of government, this will bring fair sharing of leadership. Yani ningependa tuwe na serikali ya majimbo ili tuwe na usawa katika mamlaka, kwa mfano hapa kama Municipality council, despite the fact that this District belongs to so many wanaishi watu wengi, lakini other tribes has no representatives in the Municipality council with that of county council. So there should be a Majimbo system of government.

There should be a President and his powers will be as follows. Raisi atakuwa na mamlaka kama ifuatavyo. Kwa sababu ya muda, wacha niende tu kwa major point kwa sababu nitapresent hii karatasi, itabaki hapa. There should be a Prime Minister and his Vice. There will be a governor from every region who will be elected by the native people of that region.

Interjection Com.Nunow: Tafadhali usi-transalate just present your views in whichever language you chose.

Julius: There should be boundaries of every tribe, every Kenyan can live anywhere and own land and wealth that will be protected by the government. If a person wants leadership, he can go back to his native home and ask for leadership there. I would say that, that are not allowed to ask for seats at other people's native homes.

Short people should not be discriminated during armed forces recruitment. All civil servants should be transferred anywhere country wide i.e, the MPs and the officials not decide their own salaries. Administrators from village elders to chiefs to be elected by the people and all be getting salaries. Retired officers should be not be re-appointed to any post.

Interjection Com.Nunow: Thank you we can have that memorandum and we will read every work there. Please obey the instructions, because if everybody disobeys it we will have cumulative effect and many will be left out. So thank you very much for your views so please hand in the memorandum. Seluk Josephat.

Seluk Josephat: Asante sana Bwana Commissioner, kwa majina naitwa Josephat Seluk na maoni yangu ni ya kibanafsi na pia ni maoni ambayo inaweza kusaidia wa Kenya kwa jumla. Ningependekeza, ya kwamba, atika elimu katika Katiba ya zamani ambayo tunaomba Katiba ya sasa ambayo inaenda kuundwa iwe elimu ambaye inaenda wanaenda kuuda Katiba, iwe elimu ambayo inaangalia kila sehemu. Ninaposema hivyo, ninasema kwa kushangaa kidogo kwa sababu mzungu alipokuja, alisema ya kwamba analeta elimu na pia analeta kuondoa umaskini pamoja na hata kuondoa magonjwa. Lakini ukiangalia mambo haya kwa upande mwingine katika nchini Kenya, unaona ni upande ingine unashindwa kama kuna sheria iko inaendelea mbona hiyo isianganalie kufanya follow up na kuangalia ya kwamba kuna wengine ambao hawajapata elimu, iwasaidie wale ambao wamewachwa, sasa naona ya kwamba sheria hiyo ikazwe kwa sababu kuna wale ambao hawaendelei kusoma, lakini sheria iko bona serikali haingalii?

Interjection Com.Nunow: tafadhali usiulize maswali, tupe mabendekezo kile ungependa kuiona katika Katiba mpya.

Seluk: Pia tungependa kuona ya kwamba kuwe na sheria ya kuaangalia wale ambao ni maskini na wale ambao ni matajiri, kwa sababu ukingalia matajiri na maskini unaona kuna ubinafsi saa zingine, na hio ubinafsi, pengine ile kitu ingeweza kuondoa ni ile sheria ambayo inaweza kufuatilia mambo ya tajiri na maskini kwa sababu, tajari anaendelea kuwa tajiri anaendelea kuwa tajari lakini maskini anaendelea kuwa maskini.

Lingine ningependa kuona ya kwamba hata pia heshima ingekuweko ningependelea Katiba hii, ione ya kwamba kila upande uheshimiwe kwa sababu wanajua vile walivyo. Upande wa mashamba, ningeaona ya kwamba serikali wanajua mambo mengi na wanapona watu wanaongea juu ya mashamba, wangejaribu kuona ya kwamba dawa ni hii, kwa sababu ukiangalia katika maandiko matakatifu ya Biblia inasema aombaye hupewa, na kama watu wameomba kwa haki, na kuna wale ambao labda pengine wamenyanganya, mashamba pasipokuwa na haki, basi Katiba ambayo inaenda kuundwa iweze kuangalia mahali pale.

Com.Nunow: Asante tafadhali jiadikishe pale, Wafula, Wafula njoo, John Makete, uko, jitayarishe, afuatwe na Enock Kiboi, endelea mzee.

John Wafula: Maoni yangu, nimesikia mengi, lakini nitawaelezea kidogo ndio niongezee jambo lingine. Jina ni John Wafula, ndio mimi. Kuna wenzangu waliongea mambo ya udongo, au ya mashamba. Mashamba nitaongozea yangu, hapa kweli sisi tulipigana na mzungu tangu amekuja kule Webuye kwa Chetambe, tulipigana na mzungu tulikataza mzungu asiingie katika Kenya, tukapigane naye. Kumalizika hapo, nimekuja kwa ufupi, tuliishi hapa, hapa imekuwa kabla ya kupigana na mzungu alikuwa hapo mtu anaitwa Kitale na Bidale ndio ikaitwa nani Kitale. Hapo mbeleni mtu alikuwako Nadebe ndiyo akaitwa nini, Endebes hiyo jina ni yetu Korongoro ni jina yetu, kwa hivyo sisi tulikuwako mwanzo mpaka leo ndio mnaona wanasema hawa watu wanakuja kuomba sisi mashamba. Ndio sisi hatukatai, vita ya mbili tulipigana na mzungu mwaka wa 43, mtu aliagiza hiyo vita ya kusema huyu mtu tulipigana naye mbeleni, tulizuia yeye kuingia Kenya, sasa tunapigana vita ya kufukuza yeye aende wapi ng'ambo, hata kila mtu anashuhudia mtu anaitwa Elijah Masinde, na Joash Walimoli, walianzisha tena hiyo vita 43, kuanzisha hiyo vita halafu mzungu anasema tutaua hawa watu tumalize, walishikwa 48 wakaenda, Kenyatta akarudia akasema lazima hawa wafanye nini waende tukasaidiane na wa kikuyu wazungu wakaenda. Wakatuachia udongo, sasa wengine ambao wanakuja juzi wanasema sasa huu udongo tuwagawe tu lakini wasiseme watufukuze sisi hiyo ni taabu au ni kitu kibaya.

Neno langu la pili, awe Commissioner uangalie hapo, watu wale ambao wanaweza gawia wengine mashamba wale walipigana, na mzungu kuja na kufukuza mzungu nasema asante kwa hiyo.

Neno la pili nasema watoto wa Kenya, kutoka std one mpaka University wapate masomo ya bure kwa sababu hawa watoto ni watoto, wa Kenya, ili umoja wa mataifa mkisomesha hawa watoto kweli wataona Kenya wanaendelea vizuri wazee wapate kupumua vizuri, wa kule vizuri bila kusukumwa na watoto, sasa Bwana kengele ninasema asanti sana, sitaki kupita hapo, nashukuru kwa nyinyi wote, asante.

Com.Nunow: Asante Maket Suma yuko, Tom Makete Suma yuko? Enock Kiboi, Enock are you there? Utafuatwa na Amos Buchedich. Just a minute, mzee keti tafadhali keti.zungunza tu

Enock Kimatete: Mimi naongea juu ya Trans-nzoia, Trans-nzoia hii watu wenye wako leo, wale wabukusu katika ma District ingine yote hii, tunayekuwa kati kati yao wao, kuna mkutano kama wa leo uko huko kwao. Jina Enock Kimatete, kwa hivyo wale tunayekaa leo hapa kuna District hizi zingine zote tunafuatana naye mkutano ingine inakaa kutafuta mashamba kwa District hizi zingine kama leo hapa Kitale? Tunaona tunakaa Kitale hii tunyanyaswa, ma chief wenye wako, ma sorovea na wale ma advocate wanatuingolia kwa sababu mtu anaenda kufuta shamba yake, hawa watu wananyanganya. Kwa hivyo ma District zingine zote zile tunakuwa nayo jirani wako na mkutano kama wa leo, yenye kutafuta huko mashamba, au ni hapa Kitale? Hayo ndio mimi naona ningependekeza kwa mkubwa wetu kama amekuja hapa, aone ni sababu gani na hii tangu tulikuwa na wazungu, wazungu walienda shamba tunakaa tunanyanyaswa, tunanyanyaswa, na sisi ni wabukusu tu peke yao, hakuna watu wengine wako na mashamba hii jirani wetu, hawako huko wako hapa peke yake. Yangu nafikiri ni hayo tu.

Com.Nunow: Mzee asanti tafadhali utajiadikisha hapa, Enock Kiboi.

Enock Kiboi: Commissioners wote wa Katiba walioko hapa, siku ya leo, jina langu ni Enock Kiboi. Commissioners wote walioko hapa siku ya leo kwanza narudisha shukrani kwa nyinyi kuja hapa siku ya leo kwa grassroot level, kuchukua maoni ya wananchi juu ya Katiba.

Mimi kitu cha kwanza ningesema uchaguzi wa President, terms ya office ziwe mbili. Uwezo uwe vile ulivyo sasa na mambo ya kusema tulate viti kama Waziri mkuu, hiyo haifanyi kazi kwa njia nzuri kwa sababu tulionelea nchi yetu ya jirani ya Uganda, hapo mapema walipata hicho kiti cha Wizara mkuu Bwana Kabaka sir Edward alikuwa President na Obote akakuwa Waziri Mkuu, alipata nafasi hiyo kupidua serikali, kwa hivyo tunataka President ambaye yuko na powers kamili. Nikija upande wa shamba, wakati wa koloni walipokuja nchi hii, walinyakua aridhi ya jamii fulani katika Kenya hii, na jamii imebaki kuwa wengi wao wamebaki kuwa squatters hadi wa leo. Na kwa sababu ardhi ni kitu ambacho kilikuwa kinatagemeo na wazee wetu wa zamani, it source of relief lazima waone ya kwamba jamii ambayo ilikuwa imenyakuliwa aridhi yao, sababu haikuuza, serikali wapewe hawa mashamba haza kama ni waSabaot. Hiyo ikiwa jamii moja katika nchi hii ya Kenya ambayo ilipoteza mashamba kwa wingi sana.

Jambo la mwisho ni corruption, mambo ya corruption idala kama ya Katiba iundwe kamili iwe idala ya kuchunga Katiba ifanye kazi kwa sababu tunaona immediate baada ya uhuru, Rais Kenyatta, na Jaramogi Oginga, walipitana yule ataunda KPU kwa sababu Katiba haikufuatwa, haikufanya kazi kikamilifu, corruption ilizidi katika nchi, na hiyo mzee akaunda chama cha KPU kupinga tena serikali na alikuwa Makamu wa kwanza kwa hivyo, corruption lazima iwe idara ya ku deal na corruption. Siku hizi kuandika watoto ni pesa, wewe uhongane ndio mtoto wako anaandikwa kwa kazi, wewe ni mkenya unahongana mtoto wako ana makosa gani ndio uhongane. Asante sana.

Com.Nunow: Asanti sana mzee Enock tafadhali jiadikishe, Amos Bushedich, Councilor Kobasi.

Amos Bushedich: Asante sana Commissioner majina yangu ni Amos Bushedich Balinga, ninayo machache ambayo ningependa kupendekeza. La kwanza ningependekeza uchaguzi mkuu ufananyike chini ya Katiba mpya. Jambo la pili ninapendekeza sehemu ambazo wamezitaja kuwakilisha bunge, hizi sehemu tisaini za uakilishi bungeni ziongezwe sababu tunaona tulipewa juzi chiefs, assistant chiefs Administration ikawa karibu na wananchi, kwa hivyo tukiongeza hizo Constituencies huduma itakuwa karibu ya wabunge.

La tatu, jina Trans-nzoia limekuwa jina la daraja kila mtu anarukia, anarukia anaenda tuna head quarters ya Trans-nzoia ni Kitale wapindue hilo jina Trans-nzoia liwe Kitale. Jambo la tano kwa sababu boma haiwezi kaa bila baba, President lazima awe na mamlaka yote, kushika ufunguo wa silaha ya taifa.

Jambo la sita tunaonelea serikali ya majimbo, huduma itakuwa karibu na wananchi. Jambo la saba, tulihitaji vyama vingi, sioni haja ya mtu kusema nataka chama kimoja ama viwili, hata ikifika 1,000 no problem utaenda mahali unataka, chama unachotaka. Jambo la nane, kiongozi ni lazima aheshimiwe, community yoyote kama ana kiongozi wao amechaguliwa, ni lazima sheria iundwe ya kuchunga yeye kwa sababu jamii inamtegemea.

Jambo la tisa, ninaona watu wanauliza mambo ya mashamba, Commissioner ya Njonjo imekuwa juzi tungeomba Commission iulize Njonjo iharakishe kwa sababu ni mambo ya mashamba, watengeneze hiyo Katiba ya mashamba.

Jambo la kumi, tunaona watoto wetu wanasoma wanaenda college, wanaenda Nairobi, wanaenda Kaimosi, wanaenda wapi, tungeomba shule St.Joseph High School wapinduwe iwe Teachers Training college Trans-nzoia hii.

La mwisho, wabunge wawe siku tano wakifanya kazi kwa bunge, hawa wanakula pesa mingi na hawaoni watu. Siku hizi zingine wanafanya nini? Kwa haya machache asante.

Com.Nunow: Asanti sana tafadhali jiadikishe, Councilor Kotasi, yuko Councilor?

Morris Nangole: My names are Morris Nangole, Chairman Nzoia County Council. As a Council we have the following recommendations to present to you:

We start with the executive, we should have an Executive President and then we have Prime Minister who will form a Cabinet.

Parliament, there should be some Parliamentary committees with powers which can overlook Commissions like the A-G the

Attorney General, and the Auditor General, and even supervise look after the Electoral Commission. We also said that the AG should be autonomous should be completely free from influence from the office of the President, the Election, Electoral Commission also should be very very free, to make decisions which are bidding, they should not be dictated by any higher authority.

We came down to land, we are saying that land is a very burning issue in the country, there should be a minimum number of acreage given to the people, and the minimum meaning if need be, at least five acres. Maximum should not exceed 300 acres, I think 300 is economical enough for those who are able and five acres would also be economical enough for those who have no land. We also mention something about the local government, we are saying the land act, it should be overhauled, the leaseholds, freeholds and so many other things talking about land, and the ordinary man, I am sure we do not even understand it, hatuelewi ni nini hii. Kwa hivyo simplify language, land act should be reviewed and properly written to satisfy the wananchi in general.

Also we touched on Local Government, I have heard a lot of talk about wananchi being suppressed or something like that, we are saying if we want, wananchi to survive, if you want the government the people feels, that they are in their country and the government is there we must bring back the authority to the local government. Decentralize the powers, it should be from bottom to top, but I think as per now it is from top to bottom. We have a feeling that if we decentralize the powers, bring back the powers to the people, at locals then we shall manage, create a good government for our people. The Sabaoit will be represented, Bukusus will be represented, the Kikuyu will be represented the 42 tribes will be represented at local level. In that way we think we form a better government for our people.

We also mentioned something about the powers of the DC, the administration, should be in a way scrapped it is needless to have the DCs, if we strengthen the Local Authority, then we will need police, we need health Department, we need education and all that, we will decentralize everything and then the Local Government should be supervising all these activities in the District. We are also saying that, the Chairmen should be elected by the public, we do not want where 10 people are electing a chairman every time and then we want a cross section of people, the Sengwer should elect their chairman, the Saboit, the Luhyas all over the whole country will have a say on their chairman, and like that, it will be a democratic way of doing the elections and I am sure will get good leaders. Also we are insisting on educational standards, we are saying a chairman of a county council should be a well informed person with good records, truck records behind, asiwe tu mtu wa kuokota huko, na huko halafu anakuja kuharibu a council, or a Municipal council, so we need those, and the minimum education we said, should be at least "O" level school certificate, "O" level.

We also touched on the issue of Judiciary, I think I have mentioned that, it should be very very, autonomous. Something about the office of the President, at the moment we tend to think there are a lot of sycophants people who are always surrounding the President and it has become a very expensive, you when the President comes to Kitale we have the big people the Ministers, in

Nairobi who are always with him coming with him hear. Then all the Provincial king is coming and you know like that we are spending a lot of money, it's a lot of millions of shillings, when a President comes to Kitale, for example I guess it should not be less than 20-30 million shillings, and I think that is a lot of money. Why don't we reduce that by saying, if the President is coming to Kitale, let him meet the people of Kitale only he can come with the team of 5, 6 Ministers, but then it is the people of Kitale. In most cases we have been denied a chance to get access to our President, or even, to we do not want that scene to continue in future.

Finally I have a document here and I think I will live it with you I am sorry the bell has gone and I would have talked much more, but with that I say thank you very much.

Com.Nunow: Thank you Bwana Chairman for your views, we will be happy to receive the memorandum and we will take everything there is. Alfred Bela, John Wafula Simon Chwele, to be followed Patrick Wambura,

Simon Twele: Mbele yenu kwa majina naitwa Simon Twele, Kwa hivyo nina mambo mawili, matatu ama manne, nitaongea juu yake.

Kwanza ni uraia, wakenya wote makabila 42, wawe raia wa Kenya bila pingamizi yoyote.

La pili ni kwamba uraia mwingine wa Kenya, ufuatwe na Katiba kwa utaratibu unao kubalika kama msichana wa nchi jirani kuolewa nchini, apewe uraia. Pia mgeni mwingine yeyote, achunguzwe kabla hajaandikishwa kuwa raia wa Kenya. Raia wa Kenya, Katiba ipitishwe ya kwamba ana haki ya kufuata sheria zote za nchi na pia kupata haki yake kwa usawa kama kuendesha biashara, ukulima na kupata elimu. Haki ya raia yeyote wa Kenya, na majukumu yake yategemee namna yalivyo patikana pale. Wa Kenya wawe na kitambulisho cha uraia wa Kenya pekee kinajoonyesha mahali anapoishi.

Ulinzi na usalama wa taifa: Mamlaka ya Rais kuwa Mkuu wa Majeshi yaondolowe, na badala yake Katiba iruhusu Mkuu wa majeshi awe amiri mkuu wa majeshi. Vikosi vyote vya majeshi viwe chini ya amiri mkuu wa na waziri wa ulinzi. Na usalam wa taifa uwe chini ya Rais wa nchi.

Utaratibu wa kudumisha nidhamu kati ya majeshi ni kwamba mwana jeshi yeyote asitembee na silaha baada ya kazi, na akiwa kazini asitishwe raia yeyote, na silaha hiyo pia asitumie silaha hiyo kwa kufanya uhalifu wowote.

Tume za kikatiba, tunahitaji tume za kikatiba, taasisi na ofisi nazo ni hizi. Katiba ipitishwe kuwa Tume iweko ya ma squatter. Tume ya ugawaji wa ardhi na tume ya uufisadi. Tume ya uchaguzi na tume ya haki za kibinadamu, na tume ya kushughulikia majanga bali, bali nchini. Asante kwa hayo.

Com.Nunow: Asante sana, tafadhali ukipigiwa kengele jaribu kutafuta point yako muhimu ya mwisho na useme ili baada ya

kengele usijukue zaidi ya nkuta ishirini hivi, ukitaja point la mwisho, usingoje mpaka ushikiwe microphone. Patrick Wambura, Joseph Njoroe,ajitayarishe Webwaye, Webwaye.

Joseph Njoroge: Asante sana ma Commissioners na wananchi waliofika hapa, yangu nitaenda kwa point direct. Kwanza tungependa kuanzia kwa mamlaka ya juu yaani ya Rais, Rais tungependekeza achaguliwe na wananchi ikiwa kwa kura peke yake, asichanganywe na councilors na wabunge, hiyo nikusema kwamba achaguliwe na kura zote za wa Kenya apate 50% ya kura zote. Pia Mayor achaguliwe moja kwa moja na wananchi katika Municipal, ili aweze kuwahudumia wa kazi ipasavyo. Pia ma chief na manaibu wao wachaguliwe moja kwa moja kwa sababu ndio pia nao waweza kuwahudumia wananchi ipasavyo, wasiwahudumie wananchi kikabila. Nikiongezea tena kidogo hata hawa wazee wa mitaa, wazee wa mitaa pia wachaguliwe na wananchi moja kwa moja, ili waache kula kuku za wananchi, ni hayo tu asantenti sana.

Com.Nunow: Asante sana Bwana Njoroge, jiaadikishe tafadhali. Wabwayi Wabwayi karibu mzee, twambie majina kisha utupe mapendekezo.

Wabwaye Webwayi: Asante viongozi ambaye Mungu aliwachagua hivi leo. Mimi nafulahi leo Mungu amechagua siku hii ya kupaka mafuta watu wake ambayo walikuwa wamekauka. Wabwayi Webwayi, mimi hapa ninikuja hapa kuona leo ni mpya, Mungu amechagua leo Kenya mpya, si Kenya ile zamani. Na jina Kenya lilikuja kwa ufisadi ndio mnaliona linaitwa Kenya, sababu ufisadi au ukora ndio ulifanya nchi ikageuka ambayo mnazungumzia haya. Sababu yake ni hivi nimesikia mengi ambayo wanasema ni kama uhalifu wa maneno. Si Mungu alijenga hivyo, neno lifuatalo ambayo linafanya mimi kusema hivyo, kuna ukora, hauishi katika Kenya kufuatana na viongozi ndio walijenga huu ukora. Mimi ni mkubusu nilizaliwa hapa Trans-nzoia mwaka wa 15, yale ambayo niliona ni yale ninasema na yale ambayo, niliambiwa na baba nisema, na yale ambayo na babu nisema leo ni siku ya kujenga, leo ni siku ya kuona (inaudible)wa mtu. Mimi hapa ninauliza, wewe ukileta mwanamke wako, awe wako Mungu amekupatia, tena kesho yake unafanya mwanamke wako huyo kuwa hotel? Hii nchi ambayo sisi tumekaa hapa Trans-nzoia, hapa Kitale ni mali si hivyo,

Interjection Com.Nunow: Mzee tafadhali badala ya kutupatia hadithi, tupatie mapendekezo umetumia time muda zako ikiwa unazungumzia historia, tupatie mapendekezo kile ungependa kuiona katika Katiba mpya tafadhali, kwa sababu tafadhali

Wabwiye: hiyo ndio mimi ninaenda kulenga.

Com.Nunow: tafadhali lenga hiyo nitakupatia dakika mbili zaidi, endelea

Wabwiye: na ikiwa hii maneno ambayo tunazungumza, tunazungumza kutoka kwa sheria kwa history, hii maneno ambayo tunazungumza inatokana kwa history kwa hivyo mimi nitasema pendekezo na history pamoja sababu yake ni hivi, mubukusu kutoka mwaka 1885 alipigana vita kwa nchi ya Kenya East Africa, alikuwa mkubusu, makabila ambayo mnasema 42 hii

ilikuwa wapi? Na mkubusu peke yake ndio alipigana. 1895 tena vita ilishuka Mbukusu akapigana hiyo vita, peke yake kwa Kenya, East Africa makabila 42 yalikuwa wapi? Mwaka wa 48 mbukusu alipigana vita Msabwa na makabila hayo 42 yalilikuwa wapi? Mwaka wa 63, waKalenjini washtaki wa Bukusu kwa CNC, CNC ikapeleka case kwa bunge, bunge ikapeleka kwa Bruce Mackenzie hiyi case ilifanyika na wa Bukusu, nani alikuwa 42 hawo walikuwa wapi? Sasa wakati huu kusema mkubusu hawezi kuzungumza sababu akizungumza, sisi hatutakunywa humu hotel, tunataka mtufunike sisi tusiwe wenye nchi, sasa yule ambaye anasema nchi hii ni yake, atambue sababu yake na mimi nitambue sababu yangu mbele ya watu wa Mungu, na mbele ya viongozi wa Kenya.

Com.Nunow: Asante sana mzee tafadhali jilandikishe pale, Mary Nasimiyu, tafadhali, tafadhali, tukimie tusikize.

Mary Nasimiyu: Majina ninaitwa Mary Nasimiyu Wanyonyi, mkaazi wa hapa Kitale na mzaliwaji wa hapa. Yangu ni mawili, matatu hivi kwa sababu sisi ndio tulizaliwa hapa Trans-nzoia. Nimeona watu wanaongea upande wa mipaka sana na upande wa ukabila, sisi ndio wale tulizaliwa hapa, tunahangaikia hapa, hatuna makao tunakaa kama wa mama hapa, wazazi wetu walikufa wakatuacha hapa, na sisi kweli hatuna makao hapa hata kidogo hapa Trans-nzoia. Sasa ninashindwa mtu akitoka mbali anaanza kulia mambo ya mipaka, mambo ya mashamba, na sisi wenyewe tumefanyia ADC kazi, ukifanyia ADC kazi hakuna mshahara, wanakwambia kama unataka mshahara chukua chakula, na chakula tutasomesha watoto namna gani? Kama wamekupatia mahindi debe moja, unaweza kuuza halafu upeleke mtoto wako shule? Watoto wetu wanahangaika sana, hawana masomo wanafanyia watu kazi na mbali sisi wenyewe hatujiwezi. Sasa sisi tunaomba Katiba ya saa hii ingangalie wa mama kama sisi kweli sisi wa mama tunahangaika sana, hapa Trans-nzoia. Unakuta mtu anashamba kubwa sana lakini una mfanyia kazi anataka akunyanyase na bali uko na watoto. Jee watoto wa wamama kama sisi, watasoma ama hapana tunataka Katiba ituangalie mambo kama haya. Yangu ni haya na Mungu awabariki.

Com. Nunow: Asante tafadhali ujilandikishe, Ubio Alfonse, Alfonse Obiyo Christinos Mwasombe, who is this, Obiyo utafuatwa na Chrispinos Mwasombe.

Moses: My names are Moses Kimaiyo Bito,

Com.Nunow: I did not call you I am sorry, please keep down the Mice, we are not doing some funny games here, if I call you your names then you come, otherwise we will not have any order is Chrispinose Mwasombe here, Peter Wafula are there? Buduki Koness. Ajitayarishe Fred Kwanusu.

Bunduki Koness: Mwenyekiti, tunakukaribisha hapa kwetu, nina maneno mawili tu ambaye ningependa tu kuongeza kwa yale ambayo watu wameweza kusema. Jina langu ni Bunduki Koness, kitu ambacho ningependa kuzungumzia yani juu ya election au uchaguzi, uchaguzi ni lazima mtu ambaye anaishi mahali hapo, achaguliwe yani mwenyeji indigenious people must be elected from a place, especially hii ni ku minimize wale watu ambaye ni wachache kunyanyaswa. Haya mambo ya kusema ya kwamba

ni wingi wa watu ni lazima ndiye atakaye kwenda Parliament au awe kiongozi, sehemu ambayo kama Trans-nzoia haiwezi kutumika vizuri, kwa sababu wenyeji wanaumia. Kwa hivyo napendekeza hivi, lazima iwepo electoral college ambapo, delegates au wajube wanahuzika. Hatusemi wenyeji wa area hapo, wawe na watu delagate ishirini na wahamiaji wote au immigrants, wawe na wajumbe tano. Ili waende electrol college wachague mjumbe ambaye ataakilisha hao wa indeginous people. Lakini kama sheria inaruhusu au serikali kuruhusu immigrants kutawala wale watu wengine, kwa sababu ni wachache, ni haramu. Hatuko fair kwa sababu watu wengine wamefunga mahali pao sawa sawa na wanawakilisha watu wao sawa, sawa, kwa nini tunaumiza watu wengine? Kwa hivyo sheria itungwe vizuri, kwa sababu itatusaidia, hatutaki matatizo Kenya kwa sababu tumeona mfano, kama Cambodia au wapi, hatutaki yaje Kenya hapa kwetu, tuishi vizuri.

Kitu cha pili, nazungumza juu ya citizenship, uraia, Katiba yetu ambaye tunafanyia sasa marekebisho, inaongea juu ya mtu ambaye anatoka nje anataka uraia wa Kenya, lakini haizungumzi kuhusu watu ambao waliondolewa kutoka Trans-nzoia kama wa Sabaot ambao wako nje huko vile watakuja, mwaka wa 1990, wa Sabaot walikusanyika kule Busia wengi sana wakitaka kuingia ndani, lakini walikatazwa kwa sababu ya kwamba walikuwa wengi kule. Walakini, tulijua ya kwamba sheria or Katiba hajia include hao watu ambayo wako nne. Ningependa hii Katiba ambayo sasa mnaitunga kuingiza hawo watu wetu ambaye uko nje warudi hapa Kenya. Inasemekana hata katika historia, ya kwamba wa wayahudi walikuja Ethiopia mwaka wa 1200 BC, wakati Yesu hajazaliwa, lakini juzi, wamerudi kwao sisi wa sabaot kama watu wengine hawapendi tunataka watu wetu wa sabaot warudi Kitale. Asante.

Com.Nunow: Asanti sana, tafadhali jiadikishe, Fred Kwarusu, tafadhali tusikizane, Fred Kwarusu, kama Fred hayuko Elim Orot, ajitayarishe Kalebe Ebuye.

Elimon Orot: Asante sana Commissioner kwa jina naitwa Elimon Erot, mkaazi wa Kitale, hii ni sub-Trans-nzoia kwa sababu Trans-nzoia ni jina lilikuja juzi. Mapendekezo ambayo nataka kupendekeza ama kuuliza, wa mama 42, katika jamuhuri ya Kenya wa mama 42 nyinyi wa Kenya bado mko hapa, itamburike ama isitamburike. Ninapendekeza ya kwamba kila mama atamburike kwa boma yake, ambaye hata hapa mahali mimi ninazungumzia kama ma Turkana, ninatambua hapa niko kwa mama yangu anaitwa msabaot. Kwa sababu ukweli humaanga kama nyoka. Ninasema namna hiyo kwa sababu mimi saa hii kama nateremkwa na wa Kenya wenzangu katika Kainuk mimi siwezi kukubalika wengine wakisema huko ati mimi huko Kainuk ni kwetu, nitakubali kweli? Basi mimi nitakatia hiyo hapo.

Bwana Commissioner, kwa kumiliki ardhi katika jamuhuri yetu, population yetu imezidi kwa sababu ya corruption, imezidi kwa sababu ya corruption, mimi nitaomba, tume hii iangalie vizuri, ingalie kwa sababu sisi robo tatu kama wa Kenya, yote hatuna mali pa kulala kweli kabisa. Na hapo ndio mimi nitaomba, tume hii hata kama ni kurudia kuhesabu wa Kenya, wale ambayo kabisa wako ndani halisi, kweli haiwezi kuwa kama milioni 20, itakuwa saa ingine million 15, wale wanakaa kwa ardhi kabisa.

Kwa upande wa elimu, mimi nitapendekeza hivi, kutoka std one mpaka form four, serikali yetu ya Kenya itusaidie, uwe free

kabisa. Nikimaliza mapendekezo yangu, upande wa ugonjwa, ugonjwa unazidi kwa sababu ya nini? Dawa zetu kwa Jamuhuri ya Kenya inaenda kwa ma Chemists lakini District mahali ma Dakatari wako hazitufikii kabisa, haitufikii sisi. Kwa hivyo mimi ningependekeza dawa kwa Jamuhuri ya Kenya akipita imulikwe na serikali itusimamie, ili ugonjwa uwe mbali na sisi. Kwa hivyo mimi namalizia hapo, kwa ufupi hivyo sitaki story mingi.

Com.Nunow: Asante Bwan Erot, Caleb Ebuye,

Caleb Ebuye: Asante sana Commissioner kwa kunialika hapa pendekezo yangu iko hivi.

Interjection Com.Nunow: Majina tafadhali.

Caleb Ebuye: Kwa jina ni Caleb Ebuye, ningependekeza hivi, kwanza ningependa serikali iangalie mambo ya prisoners, watu huwa wanashikwa na wanawekwa pamoja na watu wenye wabaya sana na wale wenye hawajafanya makosa makubwa, wanawekwa kwa cell moja, wanawekwa pahali moja na hiyo si vizuri, watu wachunguzwe na makosa kidogo mtu apewe bond akae nyumbani aende kortini, kuliko kuwekwa ndani ati amekunywa pombe au nini, hiyo si vizuri. Na mama mwenye mtoto hatafikani awekwe kwa cell na mtoto, kwa sababu mtoto hana hatia, mtoto anaumia bure na hajafanya lolote.

Ya pili, MPs ningependekeza MP akiwa elected asifike katikati a defect, kwa sababu yeye analeta hasara kwa serikali.

Ya tatu mtu mwenye civil servant wa serikali hatafikani afanye kazi ingine ya private, afanye kazi yake yenye ameandikwa na serikali.

Ya nne voting, voting ifanywe kwa vituo vya kwenye wanapigia kura, na hesabu ifanyiwe huko, isibebwe kupelekwa mahali pengine. Na Mayor awe elected na raia, na kwa upande wa wakulima, ningependekeza serikali isaidie mkulima ajenge nchi hii impe loan, kwa sababu economy ya Kenya imeanguka kwa sababu wakulima wamerudi chini. Kuna middlemen wenye wameingilia inputs ya wakulima hawa inputs inafika Mombasa kama mbolea, wakulima wenyewe wa import vitu kwa mpango fulani na vitu hivi vije kwa bei ya chini na itakuwa vizuri. Na tena tuwe na market nzuri ya vitu vya wakulima.

Na ya mwisho, ningemba serikali ifikirie compensation ya clashe victims asanti.

Com.Nunow: Asante tafadhali ujiandikishe, Elijah Muraya, Elijah Muraya, ajitayarishe Councilor Kauka Pius,

Elijah Muraya: Honourable Mr.Commissioners, ladies and gentlemen

Interjection Com.Nunow: tafadhalini subiri kidogo,

